## ITHIBATI YA MSIMAMIZI

Aliyetia sahihi hapo chini anathibitisha kuwa amesoma kazi hii inayoitwa "**Hali ya Kupendwa kwa Nyimbo za Injili kama Fasihi Pendwa: Mfano Nyimbo za Christina Shusho**" na anapendekeza kuwa Chuo Kikuu cha Dodoma kikubali kupokea tasinifu hii: katika kukamilisha masharti ya Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

…………………………………….

DKT. E. SONGOYI
(Msimamizi)

Tarehe:...........................................

# IKIRARI

# NA

# HAKIMILIKI

Mimi, **Happiness W. Bitababaje**, nathibitisha kuwa tasnifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa na haitawasilishwa katika chuo kikuu kingine kwa ajili ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili au Shahada nyingine yoyote.

Sahihi ………………………………………

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa njia yoyote ile, iwe ama yote au sehemu ya tasnifu hii, isipokuwa kwa shughuli halali, kwa ajili ya utafiti, kujisomea au kufanya marejeleo ya kitaaluma bila ya kibali cha maandishi ya Mkuu wa kurugenzi ya Taaluma za Uzamili kwa niaba ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

## SHUKRANI

Kama ilivyo kawaida, kwamba tasnifu inabeba jina la mtu mmoja, lakini ni ukweli usiopingika kwamba ni matokeo ya kazi nyingi mchanganyiko za watu wengi. Siyo rahisi kuandika kwa undani mchango wa kila mtu aliyenisaidia mpaka nikafanikiwa kukamilisha kazi hii. Lakini wafuatao wanastahili shukrani zangu za kipekee.

Kwanza kabisa, ninamshukuru Mungu kwa kuwa nami kipindi chote cha masomo yangu, pia kwa kuniwezesha kukamilisha kazi hii. Kwa uweza wake nilipata nguvu na uelewa wa kufanya huu utafiti. Pia, ninatoa shukrani zangu za pekee kwa msimamizi wangu wa tasinifu hii, Dkt. Elias M. Songoyi, ambaye hakusita kunishauri katika hatua zote za uandishi wa kazi hii mpaka nilipoikamilisha. Asante sana Dkt Songoyi.

Utafiti huu usingefanikiwa kwa kiwango hiki kama nisingepata ushirikiano, ushauri na msaada wa hali na mali kutoka kwa mpenzi mume wangu, Ezra John Manyika, kwa kipindi chote nilipokuwa masomoni. Pia, ninawashukuru sana watoto wangu wapendwa, Innocent Bitababaje, William Mathew na Jennifer Manyika, kwa uvumilivu waliokuwa nao kipindi chote nilipokuwa nafanya utafiti huu, kwani inawezekana kabisa kuwa waliukosa upendo na malezi waliyostahili toka kwa mama yao mzazi.

Pamoja na hao, ninawashukuru wanafunzi wenzangu wa Shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili kwa ushirikiano na ushauri walionipa katika kipindi chote cha masomo. Mapenzi yao kwangu ndiyo yaliyoniwezesha katika kukamilisha kazi hii. Sitoweza kuwataja wote ila kipekee kabisa ninashukuru Martina Duwe, Kuruthum Mazongela, Bimkubwa Ally na Bisibo Taufiq.

## TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa wazazi wangu wapendwa, baba yangu mzazi, Mchungaji Wilson L. Bitababaje na mama yangu Maureen G. Ndahani, kwa kunisomesha toka darasa la kwanza hadi chuo kikuu. Walinilea, kunitia moyo na kunihimiza kusoma kwa bidii bila kukata tamaa. Wamenipa msingi wa maisha katika dunia hii. Mungu awabariki.

# IKISIRI

Utafiti huu unahusu misingi ya kupendwa kwa nyimbo za Injili kama fasihi pendwa kwa kuangalia nyimbo za Christina Shusho. Nyimbo za Injili ni mpangilio wa sauti za kuimbwa sambamba na vitendo katika uhalisia wake ukipambanuliwa kwa gitaa na zumari wenye muonekano wa kanisa, kwa maana maudhui yake huwa tofauti na miziki mingine na ni nyimbo zinazoelezea habari njema za Yesu Kristo. Fasihi pendwa ni fasihi ambayo inapendwa na watu wengi na inaleta mvuto kwa watu wengi na inatofautiana na tanzu nyingine za fasihi.

Katika kufanikisha malengo ya utafiti, nadharia ya upokezi imetumika katika uchanganuzi wa data. Data ilikusanywa kutoka mikoa ya Dodoma na Dar es Salaam. Mbinu za usaili, ushuhudiaji, udurusu wa maandiko na majadiliano zilitumika katika kukusanya data, sambamba na matumizi ya kanda zilizorekodiwa wakati mtafiti akiwa uwandani.

Utafiti umebaini kuwa nyimbo za Injili ni utanzu mmojawapo wa fasihi pendwa katika tanzu za fasihi za Kiswahili. Tumeona kuwa nyimbo za Injili ni nyimbo zenye wapenzi wengi. hii hutokana na namna mwimbaji anavyoimba, haiba yake na uwasilishaji wake na maudhui mbalimbali yanayojitokeza katika nyimbo za mwimbaji yanayoigusa jamii.

Nyimbo za Injili kama utanzu mmojawapo wa fasihi simulizi ina mchango mkubwa katika kusana kazi za kifasihi na zina maudhui mbalimballi yanayoigusa jamii. Misingi ya kupendwa kwa nyimbo za Injili ni kitu amabacho kinahitaji tafiti zaidi za kitaaluma kutokana na umuhimu wake katika jamii. Inapendekezwa kuwa tafiti zifanywe katika tanzu nyingine za fasihi.

**YALIYOMO**

ITHIBATI YA MSIMAMIZI .......... i
IKIRARI NA HAKIMILIKI .......... ii
SHUKRANI .......... iii
TABARUKU .......... iv
IKISIRI .......... v
YALIYOMO .......... vi

**SURA YA KWANZA** .......... 1
UTANGULIZI .......... 1
1.0 Utangulizi .......... 1
1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti .......... 1
1.2 Tamko la Tatizo la Utafiti .......... 3
1.3 Malengo ya Utafiti .......... 3
1.3.1 Lengo Kuu .......... 3
1.3.2 Malengo Mahususi .......... 3
1.3.3 Maswali ya Utafiti .......... 3
1.4 Umuhimu wa Utafiti .......... 4
1. 5 Mipaka ya Utafiti .......... 4
1.6 Kiunzi cha Nadharia .......... 4
1.7 Hitimisho .......... 8

**SURA YA PILI** .......... 9
MAPITIO YA MAANDIKO .......... 9
2. Utangulizi .......... 9
2.1 Mapitio ya Maandiko Kinadharia .......... 9
2.1.1 Fasihi Pendwa kwa Ujumla .......... 9
2.1.2 Nyimbo Za Injili .......... 12
2.2 Mapitio ya Tafiti Kuhusu Nyimbo za Injili .......... 19
2.2.1 Tafiti za Nje Kuhusu Nyimbo za Injili .......... 19
2.2.2 Tafiti za Ndani Kuhusu Nyimbo za Injili .......... 21
2.3 Mapengo ya Utafiti .......... 23
2.4 Muhtasari wa Sura ya Pili .......... 23

**SURA YA TATU** 24
MBINU ZA UTAFITI 24
3. 1 Utangulizi 24
3. 2 Mpango wa Utafiti 24
3. 3 Eneo la Utafiti 24
3.4 Walengwa wa Utafiti 25
3. 5 Sampuli na Usampulishaji 25
3. 6 Ukusanyaji wa Data 26
3.6.1 Mbinu za Ukusanyaji Data 26
3.6.1.1 Udurusu wa Maandiko 27
3.6.1.2 Mahojiano 27
3.6.1.3 Ushuhudiaji 27
3.6.2 Vifaa au Zana za Utafiti 28
3.7 Uhalali na Uthabiti wa Matokeo ya Utafiti 28
3.8 Uzingativu wa Maadili ya Utafiti 29
3.9. Uchanganuzi wa Data 29
3.10 Mbinu Zilizotumika Kuwasilisha na Kuchambua na Kuwasilisha Data 30
3.11 Changamoto Katika Utafiti 30
3.12 Muhtasari wa Sura ya Tatu 31

**SURA YA NNE** 32
UWASILISHAJI NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI 32
4. 1 Utangulizi 32
4. 2 Mwelekeo wa Maudhui wa Nyimbo za Injili za Christina Shusho 32
4. 2. 1 Muhtasari wa Maisha ya Christina Shusho 32
4. 2. 2 Nyimbo za Christina Shusho na Ufafanuzi Wake 34
4. 2. 2. 1 Wimbo wa “Thamani ya Wokovu Wangu” 34
4.2.2.2 Wimbo wa “Unikumbuke” 35
4.2.2.3 Wimbo wa “Ee Bwana Umenichunguza” 35
4.2.2.4 Wimbo wa “Wanifanya Ning’are”, 36
4.2.2.5 Wimbo wa “Napenda” 38
4.2.2.6 Wimbo wa “Adamu” 39
4.2.2.7 Wimbo wa “Ee Bwana Utete Nao” 40
4.2.2.8 Wimbo wa “Wastahili Kuabudiwa” 40

4. 2. 3 Mwelekeo wa Dhamira za Nyimbo za Christina Shusho ..................................... 41
4. 2. 3. 1 Wokovu ........................................................................................................ 42
4. 2. 3. 2 Hali ya Maisha .............................................................................................. 42
4.2.3.3 Imani.................................................................................................................. 43
4.2.3.4 Wema na Huruma ............................................................................................ 43
4.2.3.5 Ndoa .................................................................................................................. 44
4.2.3.6 Ukombozi ......................................................................................................... 44
4.2.3.7 Nguvu na Utukufu wa Mungu ........................................................................ 45
4.3 Upokezi wa Nyimbo Za Christina Shusho kwa Jamii ya Watanzania........................ 46
4. 3. 1 Upokezi wa Nyimbo za Injili kwa Ujumla.......................................................... 46
4.3.2 Upokezi Wa Nyimbo Za Injili Za Christina Shusho.............................................. 48
4.4 Sababu za Kupendwa kwa Nyimbo za Injili kama Fasihi Pendwa ............................ 49
4. 5 Muhtasari wa Sura ya Nne ....................................................................................... 53

**SURA YA TANO** ......................................................................................................... 54
MHUTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .................................................... 54
5.1 Utangulizi ................................................................................................................. 54
5.2 Muhtasari wa Tasnifu................................................................................................ 54
5. 3 Hitimisho .................................................................................................................. 55
5.4 Mapendekezo............................................................................................................. 56

MAREJELEO.................................................................................................................. 57
VIAMBATANISHO........................................................................................................ 59

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 Utangulizi

Sura hii ya utangulizi inatambulisha usuli wa tatizo la utafiti, tamko la utafiti, malengo na maswali ya utafiti, mawanda ya utafiti pamoja na nadharia za utafiti iliyotumika.

## 1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Hivi karibuni miaka ya 1998 nchini Tanzania kumekuwa na mwelekeo mkubwa wa kupenda au kushabikia nyimbo za Injili na Muziki wake. Pia, miongoni mwa watengenezaji, wasambazaji na baadhi ya wanazuoni wanaonekana kuvutiwa na nyimbo hizo na muziki wake. Kumekuwa pia na sherehe na matamasha mengi sehemu mbalimbali nchini, ambapo nyimbo za Injili zinaimbwa na waimbaji mbalimbali wa Tanzania na nje ya Tanzania. Waimbaji wengi chipukizi, wa kike na kiume, wamejiingiza katika kuimba nyimbo hizo na wenye maduka ya kusambaza na kuuza nyimbo hizo wanaongezeka kila siku. Hili linathibitishwa na kuwepo kwa matamasha mengi ya nyimbo za Injili tofauti na zamani na kuwepo kwa ongezeko kubwa la waimbaji wa nyimbo za Injili tofauti na zamani.

Pamoja na nyimbo za Injili kuimbwa kanisani na kwenye matamasha mengi, pia wapo waimbaji binafsi ambao hurekodi na kuuza kazi zao binafsi. Mfano wa waimbaji wa aina hiyo hapa nchini Tanzania ni kama vile, Christina Shusho, John Lisu, Rose Mhando, Godwin Ombeni, kwa kutaja kwa uchache tu. Nyimbo za Injili kama fasihi pendwa kwa hivi sasa zimekuwa na waimbaji wengi na idadi yao inazidi kuongezeka kila siku. Hii ni kutokana na ushindani ambao umesababisha fasihi simulizi ya kiswahili kukua kwa haraka sana. Baadhi ya waimbaji kama vile, Christina Shusho na John Lisu wamefanya

tafsiri ya album za nyimbo zao kwa mafanikio makubwa na wameweza kupanua soko la nyimbo za injili kama fasihi pendwa na kusababisha fasihi simulizi ya kiswahili kukua.

Kuna maswali mengi yanayoweza kuulizwa kuhusu sababu za kupendwa nyimbo hizi. Je, ni kwa sababu ya mazingira ya kijamii ya wakati huu? Je, ni kwa sababu ya mtindo wa uwasilishaji (uimbaji) na haiba za wasanii wake? Haya ni miongoni mwa maswali yanayohitaji uchunguzi wa kina. Miongoni mwa tafiti zilizowahi kufanywa, hazijaangalia maswala haya kwa undani wake. Tafiti hizo ni kama vile Barz (1997, 2003) aliyetafiti suala la Muziki wa dini kutumika kama utambulisho wa jamii; Sanga (2006) aliyechunguza mabadiliko ya Muziki wa Injili kuanzia miaka ya 1980- 2005, akihusisha matukio ya kihistoria yaliyowahi kutokea nchini Tanzania. Kitundu (2011) aliyefanya utafiti juu ya athari za maendeleo ya sayansi na teknolojia kwenye fasihi simulizi, akiangalia nyimbo za ibada ya dini ya Kikristo, Tanzania. Mkallyah (2011) anabainisha kuwa uimbaji na uchezaji uliokuwa ukitumika katika miviga ya kijadi kwa sasa unatumika katika ibada za Kikristo. Mwavike (2011) alifanya utafiti kuhusu nafasi ya fasihi katika ibada za dini za Kikristo.

Zaidi ya tafiti hizo, hakujafanyika utafiti wa kina kuelezea misingi ya kupendwa kwa nyimbo za Injili. Nyimbo za Injili zinaonekana kupendwa. Uthibitisho mzuri ni namna zinavyoimbwa katika shughuli nyingi za kijamii na kuibuka kwa matamasha ya nyimbo hizo, waimbaji watengenezaji na wasambazaji wengine wa nyimbo hizo. Kwa, hiyo mtafiti ametafiti kwa nini nyimbo za Injili hupendwa kwa kuchunguza nyimbo za Christina Shusho.

## 1.2 Tamko la Tatizo la Utafiti

Nyimbo za Injili ni miongoni mwa fasihi pendwa. Kupendwa kwa fasihi pendwa kuna sababu zake. Kuna wataalamu wameangalia sababu katika riwaya na tamthiliya, lakini utafiti huu unachunguza sababu ya kupendwa kwa nyimbo za Injili kama fasihi pendwa. Kutokana na suala la sababu ya kupendwa kwa nyimbo za Injili kutoshughulikiwa kunaleta adha kwa wanafasihi na wapenzi wa nyimbo hizo kushindwa kufahamu sababu hizo. Kutokana na adha hiyo, utafiti huu ulijikita katika kubainisha sababu ya kupendwa kwa nyimbo za Injili kama fasihi pendwa mfano kutoka katika nyimbao za Injili za Christina Shusho.

## 1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa na lengo kuu na malengo mahsusi

### 1.3.1 Lengo Kuu

Kubainisha sababu za kupendwa kwa nyimbo na Muziki wa Injili kama fasihi pendwa.

### 1.3.2 Malengo Mahususi

a) Mwelekeo wa dhamira za nyimbo za Injili teule za Christina Shusho

b) Kubainisha upokezi wa nyimbo za Christina Shusho kwa jamii ya Watanzania

c) Kubainisha sababu za kupendwa nyimbo na Muziki wa Injili za Christina Shusho

### 1.3.3 Maswali ya Utafiti

a) Ni dhamira gani zimo katika nyimbo za Christina Shusho?

b) Ni nyimbo zipi za mwimbaji huyo zinapendwa na kwa kiasi gani?

c) Ni sababu zipi zinazosababisha kupendwa nyimbo na Muziki wa Injili za mwimbaji huyo?

### 1.4 Umuhimu wa Utafiti

Tasnifu hii inakuza na kupanua uelewa wa wataalam wa fasihi kuhusu misingi ya kupendwa kwa nyimbo za Injili kama fasihi pendwa. Utafiti huu unasaidia kuongeza marejeleo kwa watafiti wengine. Kwa waimbaji wa nyimbo za Injili, utafiti huu unasaidia kuelewa sababu za kupendwa kwa nyimbo hizo, kutasaidia waimbaji kutunga na kuimba nyimbo zitakazokuwa zinapendwa zaidi.

### 1. 5 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulichunguza misingi ya kupendwa kwa nyimbo za Injili kama fasihi pendwa kwa kuangalia nyimbo za Christina Shusho. Mtafiti aliteua nyimbo za injili za Christina Shusho miongoni mwa wasanii wengine wa nyimbo za Injili kwa lengo la kuchunguza misingi ya kupendwa kwa nyimbo hizo kama fasihi pendwa. Sababu ya kuchangua nyimbo za mwimbaji huyu ni kwamba mwimbaji huyu mara nyingi amekuwa akialikwa kwenye matamasha mbalimbali ndani na nje ya nchini.

### 1.6 Kiunzi cha Nadharia

Wamitila (2003) anasema kuwa nadharia ni nyenzo kuu inayosaidia katika kufikia lengo lililokusidiwa. Anaendelea kusema kuwa nadharia ni istilahi ambayo hutumiwa kurejelea kanuni au kaida za kujumla zinazotegemezwa kwenye uwazi fulani.

Utafiti huu unaongozwa na nadharia ya Upokezi. Kwa hiyo, ukusanyaji wa data, uchambuzi na uwasilishaji wake ulifanywa kwa kuzingatia mihimili ya misingi ya

nadharia hii. Nadharia ya upokezi imo katika kapu nzima la usomaji, upokezi kwa kiasi kikubwa hujiegeza kuangalia umuhimu wa msomaji au hadhira. Katika kumwangalia msomaji au msikilizaji wanaangalia namna wanavyoipokea hiyo kazi. Upokezi uliwekwa misingi na wanazuoni wa chuo kikuu cha Constans katika nusu ya pili ya karne ya 20, hii nadharia inaongozwa na dhana ya ujumi ya upokezi. Kwa mujibu wa Wafula na Njogu (2007), miongoni mwa waasisi wa nadharia hii ni Wolfgang Iser (1974, 1978), Stanley Fish (1980), James Tompkins (1980), na Haus Robert Jauss (1982)

Wolfgang Iser (1974:22) anasema, makutano ya matini na msomaji ndiyo huifanya kazi za fasihi kuwepo. Na makutano haya hayawezi kubainishwa dhahiri isipokuwa nyakati zote yanatakiwa kuwa ya kweli. Kwa kuwa hayatakiwi kutambulishwa ama na uhalisi wa matini au silika binafsi za msomaji. Kwa wanaupokezi, fasili na hisi za matini zinaonyesha mchakato wa namna upokezi wa matini unavyoingiliwa na kupokeana. Huwezi kuitenga matini na upokezi.

Haus Robert Jauss (1982) anazungumzia dhana ya upeo wa matarajio. Dhana hii ina maana kuwa mtu anapopokea kazi fulani ya fasihi anakuwa na matarajio. Matarajio hayo yana upeo au mahali maalum yanapoishia. Huhusisha amali za kihistoria, idili, ujumi na mengineyo yanayofanana na hayo. Anaendelea kusema kuwa, maana ya matini inaweza kubadilika kulingana na mabadiliko ya dunia. Upeo wa matarajio huathiriwa na utamaduni, mazingira, idili, tajiriba na uzoefu wa maisha. Katika kazi za Blockerpeter (2005:51) Jauss anaendelea kusema, kazi ya fasihi sio kitu kinachosimama pekee yake na kutoa sura ile ile kwa kila msomaji katika kila kipindi cha wakati, lakini pia sio sanamu la makumbusho linalodhihirisha asili yake ya milele. Hapa, mwandishi huyu anamaanisha kwamba fasihi ni tofauti na aina nyingine za sanaa. Kazi ya fasihi haiwezi kutoa sura ile ile kwa kila mpokezi. Kwani wakati ukibadilika na fasihi hubadilika. Kwa ujumla, upeo

wa matarajio unabadilika kutokana na nyakati lakini pia na mabadiliko ya matukio ya kilimwengu.

Naye Stanley Fish, katika nadharia hii, anatoa mchango wake kuwa fasihi nzuri ni ile iliyojikita kwa wasomaji wake, ambapo yeye alitumia wasomaji wake kupima mwitikio kwa sentensi zenye utata kwa mtiririko wa neno baada ya neno. Hapa tunaona jinsi Fish anavyounga mkono nadharia hii. Yeye anaona katika fasihi msomaji ndiye anayeweza kutoa mtiririko wa kazi ya fasihi.

Wamitila (2008) anawaunga mkono wanaupokezi kwa kusema kuwa, ni rahisi kusema kuwa tamko lolote huwa na maana tu pale linapoeleweka na anayeamua. Kitu cha msingi ni yule anayepokea ile kazi. Kazi moja inaweza kuwa na maana nyingi kwa sababu kila mpokezi atakuwa na maana yake. Hapa tunaona kuwa, hizi tofauti zinaletwa na idili, nyakati za kihistoria za watu, matukio ya kilimwengu na athari zake, pia uzoefu wa maisha kati ya mpokezi mmoja na mwingine, ambapo mambo haya yanasababisha hawa watu watoe maana tofauti za kazi za kifasihi.

Ponera (2014) anashadidia kuwa chanzo cha kuwepo kwa nadharia hii ni matokeo ya msuguano wa kifikra uliodumu muda mrefu kuhusu dhana ya ujenzi wa maana ya matini ya kifasihi. Wahakiki wa fasihi, kwa muda mrefu, wamekuwa wakivutana kuhusu ama kazi ya fasihi huwa na maana moja tu au huwa na maana tofauti. Nadharia hii, kwa upande wake, inaamini kuwa maana ya kazi ya fasihi haina sura moja tu maalum. Imani hii inatokana na kuwa kazi ya fasihi hubadilikabadilika kulingana na mpokeaji wa kazi ya fasihi jinsi atakavyongoswa na kuongozwa na hisia zake binafsi pamoja na tajiriba zake ndio husababisha kazi ya fasihi kutokuwa tuli. aendelea Hali hiyo ya kuwa au kutokuwa kwa utimilifu katika matini za fasihi haiwezi kuchanganuliwa kwa kutumia seti ya kanuni za kimaabara kama ifanywavyo kwa dhana mbalimbali za sayansi asilia. Fasihi siyo

kipengele cha sayansi asilia, ni sanaa ya maneno. Hapo ndipo litokeapo wazo muhimu la kuhitaji sana hadhira ili alikamilishe umbo la kazi ya fasihi. Hivyo, wanaopokezi humweka msomaji au msikilizaji katikati na fanani na maana ya matini ya fasihi ili akamilishe maana. Hufanya hivyo kwa kuamini kuwa msomaji au msikilizaji huwa na mawazo ya awali kuhusu matini anayopitia. Mawazo hayo hutokana na tajiriba ya msomaji au msikilizaji hupata hisi maalum. Uteuzi na upokeaji wa sanaa hushirikishwa sana na hisi kwa mujibu wa imani na nadharia za kilimbwende, hususani ya usomaji au usikilizaji wa matini mbalimbali za nyakati zilizotangulia.

Wahakiki wa nadharia hii wanazuka na aina za wasomaji kwa sababu kila msomaji anakuwa na maana yake kutokana na tajiriba na idili zake na uzoefu wa maisha. Wayne Booth ambaye amenukuliwa na Wamitila (2002), anatumia kwa mapana dhana ya msomaji mwashiriwa ambaye ni yule anaashiriwa na kazi fulani. Anaweza kuwa msomaji au msikilizaji ambaye anafahamu za kimsingi za kazi hiyo sawa na mwandishi. Inawezekana akawa na mtazamo karibu sawa kuhusu lipi nzuri na lipi baya. Fish (1980) anadai kwamba wasomaji wanapaswa kufanya mikataba ya aina fulani na matini hizo katika miktadha mbalimbali. Msomaji au msikilizaji anayetumia mkakati wa mwitikio kusoma kazi ya sanaa hufuata hatua tatu katika weledi wa kazi za fasihi.

a) Hurejelea kazi inayosomwa kwa tafsiri ili ithibitishwe kwamba kazi hiyo inaafikiana na yale yanayokumbukwa na msomaji.
b) Hubainisha jinsi miktadha ya matini isiyohusiana moja kwa moja na maandishi inavyoweza kuhusishwa na msomaji.
c) Hudhihirisha kuwa maoni ya msomaji yanafungamana na mada muhimu (Ponera 2014: 84-86).

Hivyo, nadharia ya upokezi ilitumika kuchunguza misingi ya kupendwa kwa nyimbo za injili kama fasihi pendwa kwa kuchunguza nyimbo za Christina Shusho, kwa kufuata mihimili ya Upokezi. Baadhi ya mihimili hiyo ni kama ifuatayo;

a) Kazi ya fasihi ina maana zaidi ya moja
b) Idili, uzoefu wa maisha, utamaduni, historia na mambo ya namna hiyo ndiyo hujenga upeo wa matarajio ya mpokezi.
c) Maana ya kazi ya fasihi sio tuli yaani iko katika mwendo na inabadilika kila kunapokucha.
d) Maana na uhai wa kazi inategemea maingiliano baina ya mpokezi na kazi yenyewe.

**1.7 Hitimisho**

Sura hii ilikuwa ya utangulizi imetoa maelezo ya mpango mzima wa utafiti huu. Usuli wa tatizo la utafiti na tamko la tatizo la utafiti limebainishwa. Pia, katika sura hii malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na kiunzi cha nadharia. Sura ifuatayo ni mapitio ya maandiko mbalimbali yanayohusiana na mada ya utafiti huu.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDIKO

## 2.0 Utangulizi

Katika sura hii maandiko na kazi mbalimbali zinazohusiana na utafiti huu zimepitiwa. Sura hii ina sehemu zifuatazo: maandiko kuhusu fasihi pendwa kwa ujumla, maandiko kuhusu maana nyimbo za Injili, historia ya nyimbo za Injili na mapitio ya tafiti kuhusu nyimbo za Injili ndani na nje ya Tanzania.

## 2.1 Mapitio ya Maandiko Kinadharia

Sehemu hii inapitia maandiko mbalimbali ya kinadharia, kuhusu fasihi pendwa kwa ujumla ili kuweka muktadha wa kinadharia kuelewa nyimbo za Injili kama fasihi pendwa. Pia, maandiko kuhusu maana nyimbo na Muziki wa Injili kama fasihi pendwa na kazi au tafiti zilizofanywa kuhusiana na nyimbo na Muziki wa Injili ndani na nje ya Tanzania.

### 2.1.1 Fasihi Pendwa kwa Ujumla

Fasihi pendwa ni fasihi inayojumlisha fasihi andishi ambayo inapendwa na watu, wengi na ina leta mvuto kwa watu wengi na inatofautiana na tanzu nyingine za fasihi (Gromov, 2008). Fasihi pendwa ni tofauti na fasihi nyingine kwa sababu hulenga kuwaburudisha watu sio kuwavunja moyo. Fasihi pendwa kwa sasa ni zile zinazozalishwa ama kwa kuwa tayari kwa watazamaji kusoma au ile iliyotungwa kwenye runinga au katika sinema; hii ni fasihi inayozalishwa na waandishi ambao ni wanachama wa fasihi. Mwandishi hapa anatoa sifa ya fasihi pendwa kuwa ni fasihi ambayo inaleta mvuto kwa msomaji au msikilizaji. Andiko hili linamsaidia mtafiti katika uchambuzi wake kubaini sifa mojawapo ya fasihi pendwa ambayo ni kuburudisha na sio kuvunja moyo.

Mulokozi (1996) anaelezea maendeleo ya fasihi pendwa, ikiwemo riwaya pendwa ambayo ilisababisha kuzaliwa kwa nyimbo pendwa kulingana na sehemu mbalimbali. Mkondo wa fasihi pendwa ulianzia huko marekani mwaka 1841, ilipochapishwa hadithi ya Edger Allan Poe ya The Murders in the Rule Morgue. Baadaye, mtunzi wa Kiingereza Sir Arthur Canon Doyle (1859- 1930) aliikomaza fani hii na kuifanya ipendwe na kuenea duniani kote. Hapa mwandishi amejikita katika kuelezea historia na maendeleo ya fasihi pendwa. Andiko hili linamsaidia mtafiti kujua historia na maendeleo ya nyimbo pendwa, zikiwemo nyimbo za Injili.

Madumulla (1988) anaeleza kuwa nchi ya Tanzania katika miaka ya 1980, kifasihi ilitawaliwa na fasihi pendwa, huku fasihi za kikasuku zikipungua kwa kiasi kikubwa. Kuhusu fasihi pendwa, aliona kuwa si fasihi tupu kabisa bali inasisimua, tofauti na alivyoona katika makala yake ya mwaka 1987. Aliona wasanii wanatumia ujuzi wa kisasa wa kigeni, hivyo, kuwavutia vijana wanaopenda udadisi anuai juu ya maisha, hususani jinsi ya kutumia akili na mwili vinavyojaribiwa na mitihani migumu, na hatimaye hushinda kwa namna ya ajabu. Aliona upungufu upo kwani kazi hizo humfanya msomaji au msikilizaji ahisi sehemu kubwa ya matukio ama imo ndani ya vichwa vya wasanii tu ama marudio fulani ya uhalifu wa kigeni. Kazi hizi za kifasihi ni mwigo tu, hivyo kushindwa kudhihirisha umahiri wa waandishi wetu katika kubuni kazi za sanaa zenye mawazo yao wenyewe.

Fasihi pendwa ni fasihi ambayo haikubaliani na matatizo yasiyoweza kutatuliwa. Inachukua kanuni na maadili fulani ya jumla katika jamii, kwa mfano; akili ya kawaida, mawazo na maadili. Waandishi wa fasihi pendwa ni waandishi wanaoandika juu ya matatizo yaliyopo katika jamii. Fasihi pendwa hujibu na kujiuliza maswali yasiyoweza kutatulika, inaamini kwamba binadamu anajua kitu anachotakiwa kujua ili aweze kuishi na kuendelea na safari yake katika maisha. Sifa ya fasihi pendwa ni kwamba yenyewe ina

hadhira kubwa kuliko fasihi nyingine. Hapa mwandishi amejadili sifa ya fasihi pendwa kuwa na hadhira kubwa na kusisimua. Pia, inajihusisha na kueleza matatizo yanayoikumba jamii na kuonesha ufumbuzi wake. Andiko hili linamsaidia mtafiti kujua maudhui ya nyimbo za injili yanayoendana na jamii husika.

Khamis (2007) anadai kuwa ni kawaida kwamba utanzu wa fasihi hupata mtekenyo wa mabadiliko ili kuepuka kupooza na kushindwa kushawishi kwa fikra na umbuji. Kanuni muhimu hapa ni kwamba hatimaye, chenye mwanzo kina mwisho, sharti kichoke, lazima kipoteze nguvu na msisimko wake.  Kwa mfano, mabadiliko ya ushairi wa Kiswahili ya kutotii sheria kali za arudhi na badala yake kunogea miundo huru, hii inasemekana ni kutokana na kupooza kwa sulubu zake za ndani. Lakini kwa upande mwingine, utanzu wa fasihi bila ya kuchoka au kupooza, huweza kujikuta ghafla kutoweza kuhimili nguvu za matukio muhimu ya kihistoria, kiutamaduni, kijamii, kisiasa, kielimu na hata kiuchumi, nguvu zinazokamilisha kubadilika kwake kifani na kimaudhui.  Mwandishi anazungumzia kwamba fasihi sio ombwe, bali inabadilika kutokana na jamii inavyobalika kulingana na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Andiko hili linamsaidia mtafiti kuelewa kuwa maudhui ya nyimbo za Injili hubadilika kutokana na mazingira yanavyobadilika.

Maandiko ambayo mtafiti ameyapitia yanahusiana na mada ya utafiti kwa kiasi kikubwa kwa sababu yanaelezea chimbuko la fasihi pendwa na namna fasihi pendwa ilivyosababisha kuzaliwa kwa nyimbo pendwa za Injili. Na jinsi mazingira yanavyobadilika na kusababisha nyimbo za Injili nazo zibadilike na ziendane na maisha ya kila siku ya wanadamu. Jamii hubadilika kutokana na sayansi na teknolojia ambapo husababisha pia maudhui nyimbo za Injili kubadilika kutokana na mabadiliko hayo.

### 2.1.2 Nyimbo Za Injili

Wachunguzi wa nyimbo za Injili wamekuwa na mitazamo tofauti juu ya utanzu huu wa nyimbo. Jambo hili limechangiwa na tofauti zao juu ya vipengele walivyovichambua kwa kina. Baadhi ya tofauti zao tunaziona katika kufasili maana ya utanzu wa nyimbo za Injili na pia katika kuchambua historia na maendeleo katika nyimbo za Injili kama fasihi pendwa.

Sanga (2007) anatoa maana ya nyimbo za Injili kuwa ni mpangilio wa sauti za kuimbwa sambamba na vitendo katika uhalisia wake ukipambanuliwa kwa gitaa na zumari wenye muonekano wa kanisa, kwa maana maudhui yake huwa tofauti na miziki mingine. Pia, anaendelea zaidi na kuona kuwa muziki wa Injili umechota chembechembe za muziki wa rumba, soukous, zouk, reggae, rap, taarabu na salsa (charanga). Pia uchotaji huu unahusisha miondoko ya kucheza, sauti za muziki au melodia na uimbaji ambavyo vinawasilishwa na kwaya za kanisani. Anaendelea kuona kwamba nyimbo hizi huwasilishwa na watu wengi au mwimbaji mmoja anayerekodi na kuuza kanda zake binafsi. Aidha, anaona matumizi ya neno muziki wa Injili ni neno kubwa zaidi kuliko muziki wa kwaya kwa sababu huhusisha muziki unaowasilishwa na kwaya za kanisani, pia unaweza kuwasilishwa na msanii wa muziki wa Injili pekee.

Kutokana na kuwasilishwa katika kipindi cha huduma kanisani, muziki wa Injili unawasilishwa pia katika vipindi vya matamasha ya nyimbo za Injili. Anatolea mfano matamasha yanayofanyika kila mwisho wa juma katika sehemu mbalimbali jijini Dar es Salaam. Anaendelea zaidi na kuona kwamba sababu ya maendeleo ya sasa ya nyimbo za Injili katika uzalishaji wa kanda umekuwa rahisi sana. Kwa sababu kuna ukuaji wa vyombo ambavyo vinahabarisha vikiwemo, redio na televisheni, ambavyo baadhi vinamilikiwa na makanisa. Mchunguzi huyu alijikita pia na masuala ya jinsia katika

nyimbo za Injili ambapo akiwanukuu (Askew 2000, 2002; Fargion 1999, 2000; Perullo 2005) anasema kwamba kuna ongezeko la waimbaji wanawake hata katika utanzu huu wa muziki Tanzania. Kama ilivyo kwenye Taarabu na Rap na hii inaongeza idadi ya wanawake wanaojikita katika masuala ya muziki. Katika utafiti wake aliona kuwa nyimbo zinazohusu masuala ya jinsia na hasa masuala binafsi haziimbwi katika vipindi vya kanisani. Hapa mwandishi amebainisha kuwa muziki wa Injili una maudhui tofauti na muziki mingine. Andiko hili lilimsaidia mtafiti kuweza kujua namna maudhui ya nyimbo za Injili yanavyotofautiana na maudhui ya nyimbo zisizo za Injili.

Adedeji (2004) katika uchambuzi wake *'Classification of Nigeria Gospel Music Styles'*, aliona muziki wa Injili ni muziki wa Kikristo ambao unahubiri habari njema za Yesu Kristo na unaofanya watu wengi waufahamu kupitia vyombo vya habari kama vile redio, televisheni na kurekodiwa dunia nzima na kwenye mtandao. Aliona kuwa Muziki wa Injili kwa asili` umegawanyika katika sehemu kuu mbili: kwa upande mmoja umetokana na dini ya Kikristo na kwa upande mwingine umetokana na utamaduni wa mijini. Hii ni kutokana na chembechembe za muziki wa asili ya watu fulani na mila za muziki wa kigeni. Adedeji aliona kuwa ingawa kuna makanisa yanayotumia muziki ambao umetokana na Liturujia (*Liturgy)*, makanisa mengi hutumia pasipo kuhusisha liturujia kama vile kufanya upya na shughuli za kijamii za Kikristo.

Aliendelea kusema kuwa maendeleo ya muziki wa Injili kwa upande wa Nigeria yametokana na muziki unaotumika na wazawa wa makanisa ya Pestekoste katika miaka ya 1930 na miaka ya 1960 na kuendelea. Pili, chanzo cha muziki huu ni kutokana na kutumika katika shughuli za kijamii za Kikristo kama vile harusi katika miaka ya 1920 na miaka ya 1950. Tatu, ni kutokana na kipindi cha muziki wa Injili uliokuwa unaimbwa na bendi za misheni katika kipindi cha wakoloni. Na mwisho ni shughuli ambazo zilisababisha mchango katika kukua kwa muziki wa Injili nchini Nigeria ni kujitolea

katika uimbaji kwa mtu mmoja, kwaya na makanisa yanayojitegeme kwa makundi katika Radio ELWA, Igbaja. Ambavyo vilikuwa vinatumiwa kwenye redio na television kutoka Monrovia, Liberia kuanzia miaka ya 1950. Hapa mwandishi anaelezea kuwa muziki wa Injili ni muziki unahusu habari njema za Yesu Kristo. Pia, anaelezea historia, chanzo na maendeleo ya muziki wa Injili. Andiko hili linampa dira mtafiti kuwa muziki huu unahusu habari njema za Yesu Kristo na si vinginevyo.

Kidula (2000) katika uchambuzi wake aliona kuwa muziki wa Injili ni utanzu unaofahamika kwa Wakristo; unaojumuisha mwimbaji mmoja hadi wanane. Ni taaluma inayotengeneza fedha nyingi. Pia, na imekuwa na uchaguzi wa waimbaji katika kupata mafanikio na sio katika kazi pekee wanazozipenda lakini muziki wa Injili umekuwa soko hata katika Afrika Mashariki kwa kununua nyimbo. Anajadili kuhusu maendeleo ya muziki wa Injili na waimbaji watatu ambao wamechangia katika kuendeleza na kufahamika kwa nyimbo za Injili kwa watu wengi na kuleta mafanikio katika soko la utanzu huu. Kidula akiwanukuu Anderson (1994) Ward na Wesonga (1974) ambao wanasema kuwa muziki wa Kikristo nchini Kenya ulianza kurekodiwa tangu miaka ya 1950 bila kuhusisha masuala ya uchumi. Muziki wa kipindi hicho cha miaka ya 1950 ulikuwa unatambulishwa na redio na televisheni ukiitwa “Makwaya”. Muziki huo ulionekana umechimbuka kutokana na matawi ya makanisa ya Kikristo na kusambaa Kenya kwa makundi. Kutokana na kusambaa huku, wasanii wa muziki wa Kikristo wakatokea. Mchunguzi huyu wa nyimbo za Injili akangudua kwamba kuanzia miaka ya 1990, watu wengi hawakukua kiroho na kutopewa sauti nchini Kenya na mawazo yao na tabia zao zimefanana. Hivyo, ikasababisha hata kiwanda cha kurekodi muziki nchini Kenya kuendelea kuteseka kwa kutozwa kazi zao kihalali. Hii ikasababisha hata wasanii chipukizi na wazalishaji kukosa soko nchini Kenya. Hapa mwandishi anaangalia historia

ya nyimbo za Injili na kusambaa kwake nchini Kenya. Hivyo, andiko hili linatoa dira kwa mtafiti kwamba waazilishi wa nyimbo za Injili ni wakristo wenyewe.

Barz (2003) katika uchambuzi wake wa "*Performing Region: Negotiating Past and Present in Kwaya Music of Tanzania*", aliona kwamba muziki wa kwaya umekuwa hitaji muhimu katika mdahalo wa karne kati ya ukoloni na kuwapo kwa wamisheni na utamaduni wa sehemu fulani katika Afrika Mashariki. Na leo hii mabadiliko ya utamaduni yameendelea kuwepo katika kwaya za Tanzania katika kuendeleza makubaliano kati ya ukoloni mamboleo, ukoloni mishenari. Kumbukumbu ya historia ya kurithishwa kazi katika maisha ya kila siku katika makanisa ya vijijini na mijini Tanzania. Nyimbo za kidunia na nyimbo za kuabudu za koloni la Ulaya na kipindi cha mishenari katika Afrika Mashariki zimeendelea kuwasilishwa katika makanisa ya Tanzania. Aliona kwamba kwa sasa, kwaya Tanzania zimefuata njia mbalimbali tangu uhuru katika miaka ya 1960. Njia kadhaa ni za moja kwa moja tangu mishenari ya kwanza ya Afrika Mashariki kipindi cha katikati ya karne ya kumi na tisa. Muziki na uimbaji ni sehemu ya uinjilisti ambapo kipindi cha mwanzo zilisambazwa kwa njia ya nyimbo za kuabudu. Pia, aliona kwamba leo hii nyimbo zote za zamani na sauti zake ambazo husikika katika muziki wa kwaya, nyimbo hizo zilikuwepo kati ya Vita vya Pili ya Dunia na kipindi tangu uhuru katika miaka ya 1960 na kuendelea.

Nyimbo na uimbaji wa nyimbo za dini ya Kikristo una historia ndefu duniani. Simulizi pamoja na maandiko ya kihistoria huonesha kwamba nyimbo za dini ya Kikristo zilianza pamoja na dini yenyewe. Hapo ndipo jina la dini ya Kikristo lilipoanza kutumika pamoja na nyimbo za dini ya Kikristo.

Dickson (2006: 25), anazungumzia juu ya maneno ya nyimbo za Kikristo wakati zinaanza kuimbwa, anasema:

> *The words of early Christian hymns in the first century are quoted by Peter and Paul in their letters (Ephesians 5: 19) "speak to one another with the words of psalms, hymns, and sacred songs; sing in your hearts*
>
> Maneno ya nyimbo za kikristo ya awali, katika karne ya kwanza yananukuliwa katika nyaraka za Paulo na Petro (Waefeso 5: 19). "Mkisemazana kwa Zaburi na tenzi na nyimbo za rohoni, huku mkiimba na kumshangilia Bwana mioyoni mwenu." (Tafsiri yetu).

Vilevile, katika Biblia, katika kitabu cha Wakolosai (3: 16), inaendelea kusisitizwa kuwa nyimbo za dini zinatumika katika kufundishana na kuonyana. Kinasema:

> Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote, mkifundishana na kuonyana kwa zaburi, na nyimbo, na tenzi za rohoni huku mkimwimbia Mungu kwa neema mioyoni mwenu (Wakolosai 3:16).

Hivi ndivyo uimbaji wa nyimbo za Kikristo ulivyoanza katika himaya ya Ukristo. Kutoka Yerusalemu Ukristo ulienea hata kufika Ulaya na kwingineko. Kuenea huko kulienda sambamba na nyimbo za dini ya Kikristo. Uimbaji huo wa mwanzoni ulitawaliwa na zaburi. Kufuatana na Biblia ya *New International Version* (1997:772), zaburi inaelezwa kama ifuatavyo:

> *The name "psalms" comes from the Greek translation which originally it refered to stringed instruments (such as harp) then to songs such with their accompaniment. The traditional Hebrew title is tehillium, meaning praise…even though many of the psalms are prayers; one of the collections included in the book is titled "the prayers of David son of jesse (72:20)*
>
> Zaburi" ni jina linatokana na tafsiri ya neno la Kiyunani linalomaanisha ala ya muziki wa nyuzi (kama vile kinubi) na baadaye nyimbo zilizoimbwa na viambato vyake. Kwa Kiebrania jina hilo ni *tehillium*, likimaanisha "sifa"… japokuwa zaburi nyingi ni maombi; mojawapo ya mkusanyiko wa zaburi hizo, umepewa jina la "Maombi ya Daudi, Mwana wa" Yesse (NIV 1995:772). (Tafsiri yetu)

Kwa kuwa zaburi ni nyimbo za sifa na pia zina umbo la sala, ndiyo maana zilichukua nafasi kubwa kwenye ibada za kale hapo Ukristo ulipoanza. Akizungumzia uimbaji wa zaburi huko Hispania, katika nyumba za watawa, Dickson (2006) anasema:

> *Worship in the fifth century, Psalms were always sung, those at night, through the day. Though they were not the only texts sung, they occupied the central place in the liturgy.*

> Wakati wa kuabudu katika karne ya tano, zaburi ziliimbwa mara zote, usiku na mchana. Ingawa hazikuwa nyimbo pekee zilizoimbwa, zaburi zilichukua sehemu kubwa ya liturijia (Tafsiri yetu).

Huu ulikuwa mwanzo wa kuenea kwa nyimbo za dini ya Kikristo kutoka bara la Ulaya mpaka ulimwenguni kote na kusababisha mabadiliko katika nyimbo hizo za dini. Dini ya Kikristo ililetwa bara la Afrika na wamishionari kutoka Ulaya, Williams (1972) anasema kuwa wamishionari waliokuja Afrika walikuwa na lengo la kuleta Ukristo na manufaa ya maendeleo yao ili kuwabadilisha Waafrika kimwili na kiroho. Waliweka vituo sehemu mbalimbali katika Afrika kufuatana na madhehebu ya dini zao. Wamishionari hao walikuta Waafrika wakiwa na dini zao na mitindo yao ya kuabudu. Wamishionari walitafsiri nyimbo za dini ya Kikristo kutoka katika lugha zao kama vile Kijerumani na Kiingereza kwenda lugha za Kiafrika kama vile Kiswahili, Kigogo, Kisukuma na nyinginezo na kuwafundisha waumini wao kuziimba kama walivyokuwa wakiizimba wao (Dickson 2006: 175).

Wimbo mmojawapo uliotafsiriwa kutoka lugha ya Kiingereza kwenda Kiswahili ni Rock of Ages." Ubeti wake wa kwanza unasema:

Kiingereza. ***Rock of Ages***

> *Rock of ages, cleft for me,*
> *Let me hide myself in thee,*
> *Let the water and the blood,*
> *From thy riven side which flowed,*
> *Be of sin the double cure,*
> *Cleanse me from its guilt and power* (Tenzi za Rohoni)
>
> Kiswahili, **Mwamba Wenye Imara**
>
> Mwamba wenye imara,
> Kwako nitajificha,
> Maji hayo na damu,
> Yaliyotoka humu,
> Hunisafi na dhambi,
> Hnifanya mshindi (Tafsiri yetu).

Wimbo huu ulitafsiriwa katika lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za jamii ya Watanzania.

Kisukuma: **Mimbo ga Kungongolela Muhungu**

Ikiganga cha kale,
Chatandulwa kulwa nie,
Ng'wenumo nabungila,
Umo mini'nga akinga,
Ndeke kutindwa nsango,
Mhija mu nguzujako. (Inland h.t)

Ujio wa wamishionari Barani Afrika ndio ulioanzisha historia ya nyimbo za dini ya Kikristo hapa Afrika. Kipindi hicho utunzi na uimbaji wa nyimbo uliongozwa na vifaa mbalimbali vya muziki. Nyimbo zilizotafsiriwa zilichapishwa na kuhifadhiwa vitabuni. Vitabu hivyo vilisaidia kueneza nyimbo hizo na kusababisha kuwa na waimbaji walioimba nyimbo za Tenzi za rohoni (Anderson, 1977).

Dini ya Kikristo iliingia Tanzania mwishoni wa karne ya 19. Kwa mujibu wa Anderson (1977), wamishionari wa kwanza kukaa na kuanzisha Ukristo ni UMCA ambao walinunua ardhi na kufanya makao yao huko Mbweni Bagamoyo na Zanzibar. Shirika la UMCA lilinunua eneo huko Mbweni mjini Zanzibar na kituo cha Bagamoyo kilianzishwa na watawa wa Holly Ghost Fathers mwaka 1876. Wakristo wa kwanza walikuwa ni watumwa waliokuwa wamekombolewa. Shirika la watawa wa Holly Ghost Fathers, pia lilijenga kanisa la St. Joseph lililopo Dar es salaam na waliandaa kitabu chao cha nyimbo za Liturujia kwa lugha ya kilatini. Wamishionari wa Kiprotestanti nao walianzisha vituo sehemu ya pwani, Uzaramoni na Zanzibar. Uimbaji kwa kutumia liturujia ulienea katika maeneo hayo, lakini pia juhudi za kufanya uimbaji uwe Wakiafrika zilikuwa zikifanyika. Andirian anasema; 'Juhudi zilifanywa ili kufanya uimbaji wa nyimbo za ibada uwe wa Kikristo'. Kituo cha muziki kilichojengwa na Wajerumani huko Luhijo, Bukoba, kiliweza kutengeneza muziki wa nyimbo za dini. Chuo cha Theolojia cha Makumila kilikusanya

tuni (lahini) za asili na kutungia maneno ya dini ya Kikristo ili kuandaa kitabu cha nyimbo za sifa cha *Tumshangilia Mungu* kilichohaririwa mara tatu mwaka 1973. Katika kutekeleza lengo hilo la kufanya uimbaji uwe wa Kiafrika zaidi, wamishionari pia walitafsiri nyimbo za dini kutoka lugha za kigeni kwenda lugha za makabila mbalimbali za Kiafrika. Miongoni mwa nyimbo zilizotafsiriwa katika lugha za makabila mbalimbali ni pamoja na huu ufuatao: (Wimbo wenyewe kwanza kabla ya tafsiri ya Kigogo)

Kigogo: Gwe 'Bwe mono watulwa

*Nihundikaje kwako,*
*Sakani yako yeza,*
*Miti mbeka ya itamu,*
*Yinyezeze lukulu,*
*Kanyhi umenele'ne.*

Hata leo hii tunaona kuwa wapo waimbaji wengi wanaoimba nyimbo zao kwa makabila mbalimbali na hii husababisha nyimbo za Injili au za dini zipendwe zaidi kwa sababu zinagusa jamii kubwa ya watu pasipo kubagua mtu yeyote. Vilevile, tumeona kwamba historia ya nyimbo za dini za Kikriro ndizo zilizosababisha kuwepo kwa nyimbo za Injili maana nyimbo za Injili zimetokana na nyimbo za dini ambazo lengo ni kueneza habari njema za Yesu Kristo.

## 2.2 Mapitio ya Tafiti Kuhusu Nyimbo za Injili

Wataalamu mbalimbali wamefanya utafiti juu ya nyimbo na muziki wa Injili ndani na nje ya Tanzania. Baadhi ya watafiti waliofanya tafiti juu ya nyimbo za Injili ni pamoja na:

### 2.2.1 Tafiti za Nje Kuhusu Nyimbo za Injili

Baadhi ya tafiti zilizofanywa nje ya nchi kuhusu nyimbo za Injili ni pamoja na Barz (1997, 2003). Huyu alitafiti suala la Muziki wa Dini Tanzania kwa kutumika kama utambulisho wa jamii. Alingudua kuwa muziki wa dini hutambulisha jamii husika. Hapa mwandishi anaelelezea kuwa muziki wa Injili ni kitambulisho cha jamii husika. Mchango

wake katika utafiti huu umejikita katika kutambua jamii mbalimbali kupitia muziki wa dini. Mtafiti ameweza kujua jamii husika kupitia nyimbo za Injili.

Johnson (2009) alichunguza maendeleo ya nyimbo za kidini na kiroho. Aligundua kuwa nyimbo za kidini na za kiroho zinakuwa kila siku. Hii ni kutokana na mabadiliko yanayotokea katika jamii kutokana na utandawazi. Hapa mwandishi anaelezea kwa namna gani utandawazi ulivyosaidia kukuza nyimbo za Injili. Mchango wake katika utafiti huu utasaidia kugundua mabadiliko yanayotokea katika jamii jinsi yanavyosababisha muziki na nyimbo za Injili kubadilika kutokana na utandawazi. Pia, kugusa maisha ya jamii na hii ndiyo husababisha kuwepo kwa misingi ya kupendwa kwa nyimbo za Injili kama fasihi pendwa.

Raymond (2002) anaeleza kuhusu muziki  mweusi wa Injili. anadokeza kuwa kutafsiri ya muziki wa Injili ya Amerika na Waafrika kwa kueleza historia yake na maendelea ya kimuziki kutoka mwaka 1900 mpaka 2000.  Katika utafiti wake aliweza kugundua kuwa, asili au chanzo cha muziki wa Injili wa Waafrika ulianzia Amerika. Mtafiti huyu aligundua kuwa historia ya muziki wa Injili umeanzia Marekani. Mchango wake, katika utafiti huu umesaidia kugudua historia ya nyimbo za Injili za Waafrika.

Robinson (2010) alifanya utafiti unahusu kuendeleza ufundishaji wa uimbaji wa nyimbo za Injili. Alilenga kuelewa utamaduni na vipengele vya utendaji wa sauti katika muziki wa Injili. Alingudua kuwa waimbaji wa nyimbo za Injili wanatakiwa kufundishwa kuelewa utamaduni na vipengere vya utendaji wa sauti katika muziki wa Injili.  Mtafiti anaelezea umuhimu wa kufundisha vipengele vya utamaduni kwa waimbaji wa nyimbo za Injili. Mchango wake katika utafiti huu umesaidia kuwa waimbaji wa nyimbo za Injili wanapaswa kufundishwa namna ya kutumia sauti vizuri katika uimbaji wao na kuelewa vipengele mbalimbali vya kiutamaduni.

### 2.2.2 Tafiti za Ndani Kuhusu Nyimbo za Injili

Dickson (2006) anadokeza kuwa nyimbo za msingi zilizoimbwa katika kanisa la mwanzo. Katika utafiti wake alibaini kuwa, zaburi ni nyimbo zilizoimbwa mara zote kwenye ibada ya Kikristo. Vipindi viliunganishwa na nyimbo zote 150 za zaburi ndani ya Biblia. Nyimbo hizo hazikuwa na beti. Hapa mwandishi anaonesha kwa namna gani nyimbo za zaburi ni muhimu katika ibada za kila jumapili kwa wakristo. Mchango wake katika utafiti huu umejikita katika kuchunguza msingi wa nyimbo za Injili. Hivyo, kubaini kuwa msingi wa nyimbo za Injili ni maandiko matakatifu hasa kutoka katika Biblia hususani katika zaburi.

Kitundu (2011) anaangalia athari za maendeleo ya Sayansi na Teknolojia katika nyimbo za ibada za Kikristo. Athari zilizoelezwa na kitundu ni pamoja na uhifadhi wa nyimbo za ibada za Kikristo katika kanda za gramafoni, kanda za sauti, kanda za sauti na picha na kuona picha, runinga na intaneti. Mchango wake katika utafiti huu umesaidia katika upatikanaji wa sayansi na teknolojia ambapo vimesaidia kuchambua misingi ya kupendwa kwa nyimbo za Injili kama fasihi pendwa, hususani kanda za sauti, kanda za kuona na picha na mtandao wa *youtube*. Vifaa hivyo vilimwezesha mtafiti kuweza kupata data za msingi kwa urahisi kutoka katika mitandao ya kijamii.

Kweka (2013) katika utafiti wake ulijikita katika uchambuzi wa dhamira katika nyimbo za Kikristo. Anabainisha nyimbo za aina tatu za Kikristo ambazo ni nyimbo zenye kumsifu Mungu, nyimbo za maadili; hizi huwafundisha watu kufanya mambo yampendezayo Mungu pamoja na wanadamu. Na nyimbo za Injili zenye lengo la kuwaokoa au kuwakomboa watu kutoka dhambini kupitia kwa Yesu Kristo. Hapa mwandishi anaelezea dhamira za nyimbo za Injili kwa jamii zenye maadili yenye kumpendeza Mungu. Mchango wake katika utafiti huu umejikita katika kuchunguza ni kwa kiasi gani nyimbo za Injili zinapendwa, hivyo kukidhi lengo la kwanza la utafiti huu.

Mkallyah (2011) anabainisha kuwa uimbaji na uchezaji uliokuwa ukitumika katika miviga ya kijadi kwa sasa unatumika katika ibada za Kikristo. Uimbaji katika miviga ya kijadi ulihusisha kupokezana kwa waimbaji ama watambaji. Hapa mwandishi anaelezea kuwa uimbaji na uchezaji uliokuwa unatumika katika nyimbo za kijadi kwa sasa unatumika katika nyimbo za Kikristo. Mchango wake katika utafiti huu umeonekana katika uchambuzi wa lengo la tatu ambalo ni kujua sababu za kupendwa kwa nyimbo za Injili.

Mwavika (2011) katika utafiti wake ameona kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya fasihi na ibada. Uhusiano huo unatokana na matumizi ya lugha katika ibada, ambapo fasihi hutumiwa kwenye maombi kama njia ya kuwasilisha haja za waumini kwa Mungu. Lugha itumikayo huwa ni yenye usanaa na mapambo. Mwavika ameangalia uhusiano uliopo kati ya fasihi na ibada. Mchango wake katika utafiti huu umejikita katika uchambuzi wa lugha kama msingi mmojawapo unaosababisha kupendwa kwa nyimbo za Injili kama fasihi pendwa.

Perullo (2011) anasema kuwa muziki wa nyimbo za injili hupigwa kwa mitindo mbalimbali kama vile *reggae*, *taarabu*, *dansi* na *zuku* hali inayozipa umaarufu na kukubalika kwa waumini na wasiowaumini, hivyo kuzidi kueneza Ukristo nchini Tanzania. Hapa, mwandishi anaeleza sababu ya kupata umaarufu wa muziki wa injili hii unatokana na mitindo mbalimbali. Mchango wake katika utafiti huu ni kuwa umesadia kubainisha mitindo mbalimbali ya uimbaji katika nyimbo za Injili kama fasihi pendwa. Mitindo hiyo ni pamoja mitindo ya kisasa, kijadi pamoja na aina za nyimbo ambazo ni muziki wa taratibu ambao pia unajitokeza katika baadhi ya nyimbo za wasanii mbalimbali hapa nchini.

Sanga (2011) katika utafiti wake alibainisha kuwa, nyimbo za Injili zimekuwa na wapenzi wengi kutokana na matumizi ya vyombo vya muziki. Anasema kuwa mwaka 1960 kwaya ziliimbwa bila kutumia vyombo vya muziki isipokuwa chache tu, ambazo zilitumia kinanda na baadhi ya vyombo vya jadi kama vile ngoma, zeze na marimba. Hivyo, pamoja na dhima zake za awali (kuelimisha na kuburudisha), nyimbo hizo zimekuwa chanzo cha kipato kwa waimbaji; wasanii hurekodi na kuuza ili kupata kipato. Mwandishi anabainisha wingi wa hadhira wa nyimbo za Injili kutokana na kuwepo kwa vyombo vya kisasa. Mchango wake katika utafiti huu umejikita katika matumizi ya vyombo vya muziki katika nyimbo za Injili kama fasihi pendwa ambavyo husababisha kuwepo na misingi ya kupendwa kwa nyimbo za Injili kama fasihi pendwa.

## 2.3 Mapengo ya Utafiti

Tukiyatupia jicho la kiupembuzi maandiko haya tunabaini kuwa katika andiko liyopitiwa, hakuna miongoni mwayo ambamo swala la misingi ya kupendwa kwa nyimbo na mziki wa Injili limechunguzwa kwa kina. Hivyo basi, utafiti huu ulilenga kuziba pengo hilo.

## 2.4 Muhtasari wa Sura ya Pili

Sura hii ilikuwa na mapitio ya maandiko kinadharia ambayo yameeleza fasihi pendwa kwa ujumla na nyimbo za Injili. Pia, mapitio ya tafiti kuhusu nyimbo za Injili ambapo imeeleza tafiti za ndani kuhusu nyimbo za Injili na tafiti za nje kuhusu nyimbo za Injili pamoja na mapengo ya utafiti. Sura inayofuata inafafanua juu ya usanifu na mbinu zilizotumika katika mchakato mzima wa ukusanyaji, uchambuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3. 1 Utangulizi

Sura hii inabainisha zana na mbinu hizo. Sura hii imeundwa vipengele vifuatavyo: mpango wa utafiti, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti, sampuli na usampulishaji, ukusanyaji wa data, mbinu za ukusanyaji data na zana za utafiti. Vipengele vingine ni uhalali na uthibiti wa data, maadili ya utafiti, uchambuzi wa data, mbinu zilizotumika kuchambua na kuwasilisha data, changamoto pamoja na muhtasari wake.

## 3. 2 Mpango wa Utafiti

Baradyana na Ame (2007:65) wanaeleza kuwa tafiti za kifafanuzi au kitaamuli hutumia mbinu za maelezo, ulinganisho pamoja na uhusishaji wa data dhidi ya nadharia katika kuchanganua data za kutolea matokeo. Mulokozi (2003:17) anafafanua kuwa utafiti wa fasihi una sehemu mbili; sehemu ya uwandani na sehemu ya maktabani. Hivyo, utafiti huu umefanyika maktabani na uwandani. Mwelekeo wa utafiti huu ni wa kitaamuli. Hivyo, ukusanyaji, uchanganuzi wa data, pamoja na utoaji wa matokeo ya utafiti huu unaegemezwa katika ufafanuzi wa data. Sehemu kubwa ya data za utafiti huu ni za uwandani. Hizi zimepatikana kupitia usaili, mjadala wa vikundi, ushuhudiaji pamoja na udurusu wa kimaktaba. Data za maktabani zimekusanywa kutoka katika maandiko mbalimbali yahusuyo nyimbo za Injili na fasihi pendwa.

## 3. 3 Eneo la Utafiti

Utafiti ulifanyika katika mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma. Mtafiti alichagua mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma kwa sababu ya kupata mapitio na machapisho mbalimbali katika maktaba za vyuo vikuu vya Dar es Salaam na Dodoma. Pia, ilikuwa rahisi kwa mtafiti kupata data kwa sababu ya upatikanaji wa wasanii wa nyimbo za Injili, viongozi

wa dini mbalimbali, wasikilizaji wa nyimbo za Injili, wasambazaji pamoja na waandaji wa muziki wa  nyimbo za Injili.

### 3.4 Walengwa wa Utafiti

Shulman (1988) anaeleza kuwa walengwa wa utafiti ni kundi la watu, vitu au asasi zinazoelezea kuhusu vitu vinavyofanyiwa utafiti. Katika utafiti huu, walengwa wamegawanyika katika makundi mawili, ambayo ni wango tafitiwa katika ujumla wake na sampuli iliyoshughulikiwa.

Utafiti huu unalenga makundi ya aina tano tu ambayo ni

(a) Mwimbaji teule wa nyimbo za Injili, ambaye ni Christina Shusho.

(b) Wadau wa nyimbo za Injili kama vile: wasambazaji kumi,

(c) Watengenezaji watano wa nyimbo za Injili.

(d) Wauzaji kumi wa kanda za nyimbo za Injili.

(e) Wasikilizaji kumi na watano wa nyimbo za Injili  Wakristo na wasio Wakristo

(f) Viongozi watano wa dini mbalimbali.

### 3. 5 Sampuli na Usampulishaji

Sampuli imepatikana kwa kutumia mbinu ya sampuli lengwa kwa mwimbaji teule na mbinu holela kwa wadau wa nyimbo za Injili kama waliotajwa hapo juu. Hii ni mbinu ya usampulishaji ambayo humruhusu mtafiti kuwachagua wawakilishi wa kutafitiwa kulingana na jinsi wanavyokidhi haja na malengo ya utafiti huu. Mbinu hii hukidhi haja au tafiti za kitaamuli kama huu ambayo aghalabu, hujihusisha zaidi na kutoa ufafanuzi na maelezo kuliko takwimu (tafiti za kitakwimu) ambazo huhitaji sampuli kubwa (Kothari, 2009).

Watafitiwa ambao wametumika katika ukusanyaji wa data za utafiti huu wamepatikana kwa kutumia mbinu holela kulingana na jinsi walivyokidhi haja ya malengo ya utafiti. Pia, wamepatikana kulingana na makundi yote yaundayo walengwa wa tafitiwa kama yalivyobainishwa hapo awali. Hata hivyo, vigezo kama miongozo ya kinadharia kutoka kwa wataalamu wa nadharia ya utafiti kama vile (Kothari, 2009), pamoja na asili ya utafiti wenyewe kuwa wa kitaamuli na unahusisha fasihi simulizi na jamii. Sampuli yenyewe itajumuisha yafuatayo:-

(a) Nyimbo kumi (10) kutoka kwa msanii teule Christina Shusho wa nyimbo za Injili ambazo ni: 'Thamani ya Wokovu Wangu', 'Adamu', 'Unikumbuke', 'Ee Bwana Umenichunguza', 'Wastahili Kuabudiwa', 'Umenifanya Ning'are', 'Wakuabudiwa', 'Ee Bwana Utete Nao', 'Wakuabudiwa na Napenda'.

(b) Wadau wapatao arobaini na watano (45) wa ngazi mbalimbali ambao ni wasambazaji kumi, watengenezaji watano wa nyimbo za Injili, wauzaji kumi wa kanda za nyimbo za Injili na wasikilizaji kumi na tano wa nyimbo za Injili wakristo na wasio Wakristo na viongozi watano wa dini mbalimbali walihojiwa.

### 3. 6 Ukusanyaji wa Data

Ukusanyaji wa data ulifanyika uwandani na maktabani, ambapo mtafiti ametumia mbinu mbalimbali katika kukusanya data ili kuweza kupata data sahihi zinazokidhi malengo ya utafiti huu.

#### 3.6.1 Mbinu za Ukusanyaji Data

Kothari (2009) anasema mbinu za utafiti ni hatua au njia muhimu zifanywazo na mtafiti ili kukwepa kujidanganya au kuwadanganya wengine watakaosoma ripoti zake. Hivyo, ni vyema mtafiti kuzingatia mbinu hizo. Anaendelea kuelezea mbinu mbalimbali za ukusanyaji data kutegemea aina za utafiti. Mbinu hizo ni kama vile mahojiano au usaili,

ushuhudiaji, mjadala wa vikundi, udodosaji na nyinginezo. Katika utafiti huu, mtafiti ametumia mbinu za mahojiano, mjadala wa vikundi na ushuhudiaji katika kukusanya data.

#### 3.6.1.1 Udurusu wa Maandiko

Udurusu wa maandiko yaliyo katika machapisho kama vile vitabu na pamoja na kwenye mitandao mbalimbali umemsaidia mtafiti kuweza kupata data. Manufaa ya kufanya udurusu wa maandiko ni kuwa taarifa zilizoandikwa huwa ni za kudumu, hivyo mtafiti au mtu mwingine yeyote anaweza kuzirejelea kwa uthibitisho (Kothari, 2009).

#### 3.6.1.2 Mahojiano

Mahojiano ni majibizano ya ana kwa ana (au ya simu au barua pepe), kati ya watu wawili au zaidi kwa lengo la kukusanya taarifa au maoni kuhusu suala fulani la kiutafiti lililoainishwa Mulokozi (1983). Mbinu hii imetumika kumsaili mwimbaji teule wa utafiti huu Christina Shusho wa nyimbo za Injili, wasambazaji kumi, watengenezaji watano wa nyimbo za Injili, wauzaji kumi wa kanda za nyimbo za Injili na wasikilizaji kumi na tano wa nyimbo za Injili  Wakristo na wasio Wakristo na viongozi watano wa dini mbalimbali. Njia hii ya usaili, kama asemavyo Kothari (2009), hurahisisha upatikanaji wa taarifa za kina kutoka kwa watu hata kama hawawezi kusoma na kuandika. Pia, huruhusu upatikanaji wa taarifa za kina kutokana na kumruhusu mtafiti kuuliza vipengele vya nyongeza. Data zilizotafutwa zilihusiana na kuchunguza ni kwa kiasi gani nyimbo za injili zinapendwa. Pia kubainisha maudhui yanayopatikana katika nyimbo za mwimbaji teule wa utafiti huu.

#### 3.6.1.3 Ushuhudiaji

Ushuhudiaji ni njia ya kukusanya data kwa kukiangalia kitu halisi, yaani kukiona kwa macho ambapo mtafiti anakuwa miongoni mwa watafitiwa na anashiriki katika shughuli

inayofanyika (Kothari, 2009). Mtafiti alitumia mbinu hii ya ushuhudiajia wa matukio jukwaani kwa kupata fursa ya kuhudhuria kwenye matamasha ya nyimbo za Injili. Hii ilimsaidia mtafiti kupata nafasi ya kuona ni kiasi gani nyimbo za Injili hupendwa kwa kuangalia wingi wa watu waliohudhuria, matendo na matukio na namna yalivyojitokeza jukwaani wakati nyimbo zikiwa zinaimbwa. Kutokana na uchunguzi huu mtafiti alikusanya data muhimu za utafiti huu.

### 3.6.2 Vifaa au Zana za Utafiti

Mulokozi (2003: 13) anaelezea kuwa, zana za kukusanyia data hutegemea mada, shabaha za utafiti, uwezo wa mtafiti kitaaluma na kifedha na hata kimazingira na kitamaduni. Vifaa vilivyotumika kukusanyia data za utafiti huu ni pamoja na hojaji mbili zenye maswali kulingana na walengwa, kalamu, karatasi za kuandikia kumbukumbu, kompyuta na kamera kwa ajili ya kupata picha za mnato na matukio ili kusisitiza na kuthibitisha uhalali wa data za uwandani.

## 3.7 Uhalali na Uthabiti wa Matokeo ya Utafiti

Uhalali wa utafiti ni ile hali ya utafiti kuwa na uwezo wa kupima jambo au mambo yaliyotakiwa kupimwa au kutafitiwa tu. Wakati maana ya uthabiti wa utafiti ni ile hali ya utafiti kuweza kutoa matokeo yanayoendana ikiwa utafiti utafanyika wakati mwingine, mahali pengine au hata na kufanywa na mtu mwingine kwa mada ileile. Vipengele hivi viwili vina uhusiano wa kimjalizo. Hivyo basi, ni vigumu kwa utafiti kuwa na matokeo thabiti ikiwa uhalali utakosekana (Kothari, 2009). Uhalali wa matokeo ya utafiti huu unathibitishwa kwa kutumia mbinu na zana mchanganyiko za ukusanyaji data ambazo ni usaili, ushuhudiaji, na mjadala wa vikundi. Kwa kutumia mbinu hizi matokeo pia yako na kiwango kikubwa cha uthabiti.

### 3.8 Uzingativu wa Maadili ya Utafiti

Maadili ya utafiti ni kanuni na taratibu zinazobainisha mambo yanayokubalika na yasiyokubalika katika utafiti. Zipo sababu nyingi zinazomhitaji mtafiti kuzingatia maadili ya kazi ya utafiti. Miongoni mwake ni kukuza malengo ya utafiti ikiwa ni pamoja na maarifa, ukweli na kuepuka makosa yasiyo ya lazima ili kuweza kuungwa mkono na jamii. Kushindwa kuzingatia maadili huweza kuleta madhara makubwa, siyo tu kwa binadamu bali pia kwa viumbe wengine na mazingira kwa ujumla (Shamoo na Resnik, 2009). Kwa vile utafiti huu ulihusisha watu, kila jitihada ilifanyika kuhakikisha kuwa maadili ya utafiti yanazingatiwa katika kila hatua ya utekelezaji wake. Baadhi ya maadili haya ni:

i. Kupata kibali cha kwenda kufanya utafiti wa uwandani kutoka kwa uongozi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, Afisa tawala wa wilaya za Ilala na Dodoma Manispaa, viongozi wa kata na viongozi wa mitaa na vitongoji katika maeneo ya utafiti.
ii. Kuwapa watafiti wa taarifa ya wazi juu ya utafiti ili waweze kutoa ushirikiano kwa hiari yao na waridhie kupigwa picha na kurekodiwa.
iii. Kuhakikisha kuwa siri za watafiti zinahifadhiwa wakati wa utafiti na hata baada ya utafiti kukamilika.
iv. Kuhakikisha kuwa matokeo ya taarifa ya utafiti yanakuwa niya kweli yanayotokana na mahojiano na ushuhudiaji wa watafitiwa. Hakuna fursa ya kudanganya ripoti ya mwisho ya utafiti;
v. Kutoa mrejesho (inapobidi) wa misingi ya kupendwa kwa nyimbo za injili kama fasihi pendwa.

### 3.9. Uchanganuzi wa Data

Uchanganuzi wa data za utafiti huu unazingatia nadharia ya Upokezi. Data zimechanganuliwa na kupangwa kulingana na malengo ya utafiti wetu. Kila lengo linakuwa na sehemu yake katika kipengele cha uwasilishaji, uchambuzi wa data na

mjadala wa matokeo. Mbinu ya ufafanuzi inatumiwa katika kuchambua data kwasababu utafiti huu sio wa kitakwimu.

### 3.10 Mbinu Zilizotumika Kuwasilisha na Kuchambua na Kuwasilisha Data

Kwa kuwa utafiti huu ni wa kifafanuzi, uwasilishaji na uchambuzi wa data unafanywa kwa maelezo. Mathalani, uchambuzi wa data za utafiti huu unafanywa kwa kutumia mihimili ya nadharia ya Upokezi. Data zinachambuliwa kwa kuzingatia malengo ambayo yamebanishwa hapo awali kuhusu utafiti huu. Data zilizopatikana uwandani kupitia njia za usaili, mjadala wa vikundi na ushuhudiaji zinachanganywa na kuoanishwa na zile zilizopatikana kutokana na udurusu wa kimaktaba kisha kupimwa na kutathiminiwa. Hii inasaidia kuongeza kiwango cha ubora na uthabiti wa matokeo ya utafiti. Baada ya uchanganuzi huu, matokeo yanawasilishwa kwa njia ya maelezo ambayo yanatumika kwa kiasi kikubwa. Njia nyingine zinazotumika kwa kiasi kidogo kutolea matokeo ya utafiti, ni picha na vielelezo ambazo ziko katika Sura ya Nne ya tasnifu hii inayohusu uwasilishaji na uchambuzi wa data.

### 3.11 Changamoto Katika Utafiti

Pamoja na mafanikio, utafiti uliofanyika ulikumbwa na matatizo kadhaa ambayo yalikuwa changamoto kubwa kwa mtafiti. Changamoto kuu ilikuwa ni ugumu wa kupata taarifa kutoka kwa mlengwa wa utafiti.  Hili lilikuwa ni tatizo kwani alikataa kuhojiwa kwa madai kwamba hana muda. Hata hivyo, tatizo hili lilisababisha kwa kiasi kikubwa mtafiti apate taarifa kutoka kwa watafitiwa wengine. Hata hivyo, mtafiti alijitahidi kadri ya uwezo wake kuweza kupata nafasi ya kufanya majadiliano na wapenzi wa Christina Shusho ili kupata data zake.

### 3.12 Muhtasari wa Sura ya Tatu

Sura hii inabainisha matumizi ya mbinu ya ufafanuzi wa data, inayohusisha njia ya mahojiano katika kupata data pamoja na vifaa vya kukusanyia data. Eneo la utafiti, mikoa ya Dar es salaam na Dodoma ilichanguliwa ili kupata mapitio na machapisho na watafitiwa. Data zinapangwa kulingana na malengo na maswali ya utafiti katika uchambuzi, na kupewa msimbo ili kuweka mtiririko unaoeleweka. Pia, sura hii imefafanua juu ya uhalali na uthabiti wa data pamoja na itikeli au maadili ya utafiti. Mbinu sahihi zilizotumika zinasaidia katika midajala mbalimbali huko uwandani na maktabani. Hivyo basi, uwasilishaji wa matokeo ya mjadala wa utafiti yanaoneshwa katika Sura inayofuata.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI

## 4. 1 Utangulizi

Sura hii ni uwasilishaji pamoja na mjadala wa matokeo. Imegawanyika katika sehemu nne zinazoakisi maswali yaliyoongoza utafiti huu. Sehemu ya kwanza mwelekeo wa maudhui wa nyimbo za Christina Shusho. Sehemu ya pili inajadili upokezi wa nyimbo za Christina Shusho kwa jamii ya watanzania. Sehemu ya tatu inajadili sababu za kupendwa kwa nyimbo za injili.

## 4. 2 Mwelekeo wa Maudhui wa Nyimbo za Injili za Christina Shusho

Hapa inafafanua maeneo matatu ambayo ni muhtasari wa maisha ya Christina Shusho, nyimbo za Christina Shusho na ufafanuzi wake na mwelekeo wa dhamira za nyimbo za Christina Shusho.

### 4. 2. 1 Muhtasari wa Maisha ya Christina Shusho

Christina Shusho ni mwimbaji wa nyimbo za Injili nchini Tanzania ambaye alizaliwa kigoma mwaka 1980. Ana mume na watoto watatu, wawili wa kike na mmoja wa kiume. Mume wake ni mfanyakazi wa TRA lakini pia ni mchungaji katika kanisa moja la TAG Tabata Kimanga jijini Dar es salaam. Mbali ya kuwa mwimbaji wa nyimbo za Injili, Shusho anajishughulisha na masuala ya kuuza mavazi. Pia, ni mtangazaji wa kituo cha SIBUKA, na anaendesha kipindi kijulikanacho kama Gospel Hits.

Shusho amesoma hadi kidato cha nne kisha akasomea masuala ya Teknolojia na Mawasiliano (IT) katika kituo cha kompyuta Chuo Kikuu cha Dar es salaam (UCC). Msingi au chanzo cha uimbaji wake umeanzia nyumbani maana alizaliwa katika familia ya Kikristo ambayo ilipenda kuomba na kusali. Kila Jumapili alikuwa anahudhuria shule

ya Jumapili (Sunday School) ambapo walikuwa wanafundishwa dini na huko ndiko alikojifunza kuimba. Alivyoendelea kukua, alijiona ana wito na akajaribu kuimba mwenyewe na wito wa kuanza kuimba nyimbo za Injili ulianza mwaka 2003. Baada ya kupata msukumo, hasa mwaka 2004 aliingia studio na msingi wa nyimbo zake ni neno la Mungu hata kama atatoa nyimbo kwa ajili ya jamii.

Hadi sasa Shusho ana albamu tano. Ya kwanza ni *Kitu Gani* yenye nyimbo nane. Albamu hii ilitoka mwaka 2004/2005. Ya pili ni *Unikumbuke* yenye nyimbo nane iliyotoka mwaka 2007/2008. Ya tatu ni *Nipe Macho* yenye nyimbo kumi na *Kwa Kanisa La Kristo* yenye nyimbo nane ambazo amezitoa mwaka 2010/2011 na *Umenifanya Ning'are* yenye nyimbo kumi iliyotolewa mwaka 2015. Albamu ya *Unikumbuke* aliizindua rasmi tarehe 30 Novemba 2008, ndiyo iliyofanya vizuri kwa mashabiki wa muziki wa Injili na imeendelea kufanya vizuri sana hadi sasa.

Shusho amefanikiwa kujijengea sifa kwa mashabiki wake wa nyimbo za Injili ndani na nje ya mipaka ya Tanzania kutokana na nyimbo zake kubeba ujumbe mzito lakini ukiwa katika msingi wa neno la Mungu. Umahiri wake katika kuimba nyimbo za Injili umemuwezesha kutambuliwa vyema ndani na nje ya nchi na kujinyakulia tuzo mbalimbali ndani na nje ya nchi. Mwaka 2014 alipata tuzo ya Afrika Mashariki na Kati ya mwimbaji bora wa nyimbo za Injili. Pia, alishinda tuzo ya msanii bora wa kike wa nyimbo za Injili. Vilevile, alishapata tuzo ya Meya Cup iliyotolewa nchini Kenya, Tuzo ya Injili (*Gospel Music Awards*) hapa nchini na tuzo ya Kenya Groove Music Awards aliibuka na tuzo ya msanii bora wa nje.

### 4. 2. 2 Nyimbo za Christina Shusho na Ufafanuzi Wake

#### 4. 2. 2. 1 Wimbo wa "Thamani ya Wokovu Wangu"

Huu ni wimbo unaoelezea wokovu ni kitu muhimu katika maisha ya binadamu. Mtunzi anasema:

**Ubeti 1**
Ngoja nikusimulie, habari ya kijana mmoja
Kijana mtanashati, mpole kipenzi cha wengi
Anazo sifa nyingi, lakini kuu kwake ni upendo
Siku moja alikutana na mwanamke msamaria kisimani
Kijana kamuomba maji, mwanamke nae kamuuliza
Tangu lini Wayahudi na Wasamaria tukashikamana
Kijana kamwambia ungejua mimi ni maji yaliyohai
Ungekuja kwangu unywe maji ili usiwe na kiu tena

**Hook**
Aliacha enzi na utukufu mbinguni
Akavuliwa nguo hata kifo cha aibu
Akatemewa mate ili mimi nipone heheeee Yesuuuu uu

**Kibwagizo**
Thamani ya wokovu wangu anayejua ni mwokozi wangu
Gharama ya maisha yangu anayejua ni muumba
Nikisema nimeokoka mbona hamnielewi
Nikisema nimependwa mie mbona mwanishangaa.

**Ubeti 2**
Maisha ni hazina iliyo mikononi mwa Mungu
Hakuna ajuaye salio la siku zake
Ukiona ni mzima leo hujui kesho itakuaje
Ndio maana nimeamua nikukumbushe habari za yesu
Yeye akikupenda wala hatoitoi kasoro,
Ukimpokea leo atabadili historia yako

Wimbo huu unaelezea thamani ya kuwa karibu na Mungu kwani yeye ndio mwokozi wa yeyote mwenye matatizo. Hapa mtunzi anaonesha kwa kiasi gani jamii inatakiwa kuwa karibu na Mungu katika kipindi chote cha maisha.

#### 4.2.2.2 Wimbo wa “Unikumbuke”

**Ubeti 1**
Unikumbuke babaa unapowazuru wengi naomba unikumbuke
Usinipite Yesu unapowazuru wengine naomba unikumbuke x2
Unikumbukex3, Yesu naomba unikumbuke

**Ubeti 2**
Maisha yangu, kazi yangu kuketi kwangu, nakuondoka kwangu unikumbuke
Mnyonge mimi dhaifu mimi (unikumbuke)
Ona huyu asie na kazi (unikumbuke)
Yatima na wajane wanalia (unikumbuke)
Kijana huyu ataka mwenzi (umkmbuke)
Na mwingine huyu ataka elimu (unikumbuke)
Umasikini sasa ndio wimbo (unikumbuke)
Nchi nzima vilio vimejaa (unikumbuke)

**Kibwagizo**
Shida zetu Mateso yetu
Usitupe (utukumbuke)x3
Serikali yetu na viongozi (uwakumbuke)
Waongoze nchi kwa hekima yako (uwakumbuke)
Uchumi wa nchi yetu (uukumbuke)
Bunge letu na mahakama (ulikumbuke)
Ona vilio vya watanzania (utukumbuke)
Majibu ya matatizo yatoke kwako (utukumbuke)
Ajali nyingi twazika wengi (utukumbuke)

Wimbo huu unaelezea kuhusu maisha ya mwanadamu kuwa yako mikononi mwa Mungu. Mwimbaji anaona kuwa suluhisho la matatizo ya wanadamu anayokumbana nayo ni kumwomba Mungu amkumbuke katika kila hali. Anasema kuwa, Mungu ndiye kiongozi wetu hapa duniani hana budi kutukumbuka, viongozi wa serikali na watu wote duniani.

#### 4.2.2.3 Wimbo wa “Ee Bwana Umenichunguza”

**Ubeti 1**
Ee Bwana umenichunguza na kunijua
Wewe wajua kuketi kwangu nakuondoka kwangu
Umenifahamu wazo langu, tokea mbali
Umepepeta kwenda kwangu na kulala kwangu
Umeelewa na njia zangu zoote
Umepepeta kwenda kwangu, nakulala kwangu
Umeelewa njia zangu zoote.

**Kibwagizo**
Hamna neno ulimi mwangu
Usiloju kabisa Bwana
Umeninzigira nyuma na mbele, ukaniwekea mkono wako
Maarifa haya niyaajabu, yanishinda mimi,
Siwezi kuyafikia, hayadhihiriki
Siwezi kuyafikia
Niende wapi nijiepushe, na roho yako
Niende wapi, niukimbioe uso wako
Kama ningepanda mbinguni, wewe uko
Ningefanya kuzimu kitanda, huko nako uko
Kama nikisoma hakika giza utanifunika
Giza nalo halikufichi kitu
Giza na mwanga kwako nisawasawa

**Kibwagizo**
Ee Mungu unichunguze, ujue moyo wangu
Ee Mungu ( ee Mungu ee Mungu)
Unijaribu, uyajuye mawazo yangu
Ee Mung (ee Mungu)
Eeh Mungu (uone kama)
Uone kama iko njia iletayo majuto ndani yangu ( ee Mungu)
Uniongoze katika njia ya haki milele
Maana wewe ndiwe uliyeniumba uzima wangu
Macho yako yaliniona kabla sijakamilika , ee Mungu
Uisikie sauti yangu (nikuitapo Baba)
Ee Mungu
Ee Mungu unichunguze, ujue moyo wangu
Unijaribu, uyajuye mawazo yangu
Maneno ya kinywa changu, na mawazo ya moyo
Yapate kibali mbele zako
Ee mungu

Wimbo huu unaelezea jinsi Mungu anavyotuchunguza maisha yetu, anatujua na anatuona kila tunapokuwa. Aidha, unaelezea kuhusu uweza wa Mungu. Pia, wimbo huu umetokana na maneno matakatifu kutoka katika Biblia kweye kitabu cha Zaburi ya 139. Hii inathibitisha kuwa nyimbo za Injili hutokana na maneno matakatifu kama tulivyoona katika maandiko mbalimbali tuliyopitia.

#### 4.2.2.4 Wimbo wa “Wanifanya Ning’are”,

Ni wimbo unaoelezea uzuri wa mtu kuwa na Mungu na kumtegemea. Wimbo huo unaelezea uzuri wa kuwa na Mungu.

Wanifanya ning’are

Aah! Damu ya Yesu
Imenifanya ning’are
Still nang’ara

**Kibwangizo**
Umenifanya ning’arex2
Umenifanya ning’are Yesu
Eeh!
Umenifanya ning’arex2
Wewe umenifanya ning’are
Yesuuuuu!

**Ubeti 1**
Wewe waitwa nuru
Eti nuru ya watu
Ukiingia kwangu mi nang’ara
Ndani ya hiyo nuru
Eti kuna uzima ukiingia kwangu nina uzima,
Haleluya kumtumikia Mungu kunafaida

**Ubeti 2**
Uso wake Yesu
Aliyesura yake Mungu
Umeingia kwangu
Mi nang’ara
Nuru ya injili
Utukufu wake Kristo
Umeingia kwangu
Minga’ara

**Ubeti3**
Inuka ungaze wewe
Nuru yako imekuija
Utukufu wa Bwana
Umekuzukia wewe
Mataifa watakujia wafalme watakuja
Utukufu waBwana
Umekuzukia wewe wanga’ra

Wimbo huu unaelezea faida za kumtumikia Mungu. Maneno yaliyomo katika wimbo huu yanahamasisha watu kuishi maisha ya kumtegemea Mungu na kuwaelemisha kuwa kumtegemea Mungu kuna faida.  Ukimtegemea Mungu atakufanya uonekana bora hata kwa watu waliokuwa wanakuona hufai au huna mchango wowote katika jamii.

#### 4.2.2.5 Wimbo wa "Napenda"

Wimbo huu unaelezea namna mtu anavyopenda na kufurahia baraka ambazo Mungu anawatendea watu wake. Mtunzi anasema:

**Ubeti 1**
Napenda nione ukinitendea
Napenda nione ukinibariki
Napenda nione ukiniinua
Kila kitu kwako mimi napenda

**Ubeti2**
Napenda nione ukiniponya
Napenda nione ukinifariji
Napenda nione ukiniinua
Kila kitu kwako mimi napenda

**Kibwangizo**
N apenda, napenda kila kitu kwako mi napenda
Napenda oo napenda kila kitukacho kwako  mimi napendax2
**Solo**, yesu we napenda, mambo yako nayapenda

**Ubeti 3**
Napenda neno lako
Napenda hekima zako
Napenda sifa zako yesu
Kila kitu kwako mimi napenda

Napenda hukumu zako
Napenda huruma zako
Napenda rehema zako
Kila kitokacho kwako mimi napenda

Wimbo huu huelimisha jamii kuhusu kila kitu kinachotoka kwa Mungu ni kizuri. Baraka anazobariki watu wake ni nyingi mno kiasi kwamba mtu huona raha na fahari kuwa na Mungu katika maisha yake. Mungu ni Mungu wa huruma, anahukumu kwa haki hana upendeleo na amejaa hekima nyingi ambazo hakuna mwanadamu aliyenazo. Jamii inaaswa kufurahia na kupenda kila kitu ambacho Mungu anawabariki na kuwapa, wimbo huu huwavuta watu wengi kumtafuta Mungu.

#### 4.2.2.6 Wimbo wa "Adamu"

Katika wimbo huu unahusu mafunzo juu ya wanandoa na wanaojiandaa kuingia katika ndoa, kuishi maisha ya kuchukuliana na kusameheana. Kwa maana wote ni wanadamu na cha zaidi, wapendane maana upendo hustili wingi wa dhambi na upendo hauna kinyongo. Mfano wa wimbo wa "Adamu" unasema:

**Ubeti 1**
Mungu alipomuumba adamu, hakumuacha awe pekee yake
Akamfanyia msaidizi wa kufanana naye, nyama yake katika nyama yake
Mifupa yake katika mifupa yake x2

**Ubeti 2**
Mwanamke ataacha wazazi wake, ataandamana na mume
Mwanaume ataacha wazazi wake, ataandamana na mkewe
Hao wawili watakuwa mwili mmoja, wanie mamoja washirikiane kwa umoja x2

**Kibwagizo**
Nakupenda
**Solo**; Mpenzi wangu umeumbika
**Wote**; Nakupenda
**Solo**; Katika viumbe umezidi pia
**Wote**; Nakupenda
**Solo;** Nimekuchangua uwe wangu
**Wote**; Nakupenda
**Solo**; Kifo tu kitutenganishe
**Wo**te; Nakupenda
**Solo**; Nikikukosea unisamehe
**Wote**; Nakupenda
**Solo**; Mi nimwanadamu wala si malaika
**Wote**; Nakupenda
**Solo**; Nakupenda mpenzi wangu.

Hapa mwimbaji anawaasa wanandoa wanatakiwa kuishi katika upendo maana wakiwa na upendo watakuwa na familia yenye upendo. Upendo ukiwepo huwezi kumwona mwenzako kama anakosea maana upendo utakufanya uwe na roho ya msamaha. Kwa hiyo, wimbo huu huiasa jamii kuishi maisha ya msamaha na upendo. Mara nyingi wimbo huu hupigwa katika sherehe za harusi na unaendana na hali halisi ya maisha ya sasa ambapo matatizo ya wanandoa ni mengi na hivyo katika wimbo huu tunapata ujumbe wa kusameheana ili kuishi maisha yanayompendeza Mungu.

#### 4.2.2.7 Wimbo wa "Ee Bwana Utete Nao"

Wimbo huu unahusu Mungu anavyopigana vita kwa ajili ya watu wanaomtumikia. Mungu hupigana vita na adui za watu wake wamchao, anawatia moyo kuwa vita ni vya Bwana na si vya wanadamu. Wimbo unasema:

**Ubeti 1**
Ee bwana utete nao wanaoteta nami
Upigane nao wanaopigana name x2
Uishike ngao na kigao
Usimame unisaidie
Uutoe na mkuki
Uwapige wanaonifuata x2

**Ubeti 2**
Uimbie nafsi yangu
Mimi ni wokovu wako
Waambishe, wafedheheshwe
Wanaoitafuta nafsi yangu
Warudishwe nyuma
Wafadhaishwe
Wanonizushia mabaya x2
Wawe kama makapi
Mbele ya upepo
Malaika wa Bwana
Akiwafuatia x2

Wimbo huu unaasa jamii kuishi vizuri na adui zao kwakuwaonya na kuwaelimisha kuwa hawapaswi kungombana bali wamuache Mungu ashughulike na apigane na adui zao. Kupitia wimbo huu tunaona kuwa unahamasihs amani kati ya mtu na mtu. Mambo haya ni maisha halisi wanayoishi watu katika dunia sasa. Kwa hiyo waimbaji wa nyimbo za injili wanasaidia kuwaelimisha jamii juu ya kuishi kwa amani na upendo na waache mafarakano bali vita vyao wamwachie Mungu atawapigania.

#### 4.2.2.8 Wimbo wa "Wastahili Kuabudiwa"

Wimbo huu unahamasisha watu kuweza kujua ukuu wa Mungu kuwa, ndiye anayestahili kuabudiwa na kuheshimiwa peke yake hapa duniani. Mtunzi anasema:

**Ubeti 1**
Wakuabudiwa, wakuheshimiwa niwewe Mungu

Wakupewa sifa, nautukufu ni wewe Mungu
Mungu mwenye nguvu, wastahili heshima zote
Hakuna mwingine,wa kulinganishwa na wewe Mungu x2

**Ubeti 2**
Umesema wewe jina lako ndipo alipo Mungu
Unafanya mambo yaliyojuu ya fahamu zetu, Mungu
Wewe unatupa kushinda na zaidi ya kushinda
Unatupandisha utukufu hadi utukufu Mungu x2

**Ubeti 3**
Uzima wetu uko mikononi mwako Mungu
Unawapa nguvu, wanyonge nawadhaifu Mungu
Mwanadamu nani wa kulinganishwa na wewe Mungu
Nani mwenye nguvu wa kusimama mbele yako Mungu x2

Kwa upande wa wimbo huu unahusu kuelimisha na kufunza jamii juu ya uweza wa Mungu ambaye ndiye anayestahili kuabudiwa na kuheshimiwa. Kila kitu alichokuwa nacho mtu ni kwa uweza wa Mungu, hakuna awezaye kufanikiwa bila kuwa na uweza wa Mungu.

### 4. 2. 3 Mwelekeo wa Dhamira za Nyimbo za Christina Shusho

Kazi ya fasihi hukamilishwa kwa mambo mawili ya msingi ambayo hushirikiana na kukamilishana katika kuijenga fasihi na kuipa muonekano wake wa kifasihi. Mambo hayo kwa pamoja huitwa vipengele vya fasihi ambavyo ni fani na maudhui. Ili msanii aweze kuwasilisha vizuri ujumbe wake kwa hadhira huitaji maarifa zaidi katika kutumia vipengele hivi ili kuwasilisha ujumbe kwa namna alivyokusudia iwe. Katika vipengele hivi vya fasihi tutaangalia kipengere cha dhamira katika nyimbo za christina Shusho.

Dhamira ni ile jumla ya maana anayoivumbua mwandishi aandikapo, na jumla ya maana anayoitambua msomaji katika usomaji wake. Dhamira hutumiwa kurejelea mada ya kazi fulani au ujumbe au lengo la kazi hiyo. Katika dhamira kuna mafunzo mbalimbali yaliyomchochea msanii kutunga nyimbo (Wamitila, 2002). Dhamira zilizojitokeza katika nyimbo za Christina Shusho ni kama zifuatazo:

#### 4. 2. 3. 1 Wokovu

Wokovu ni hali ya kusalimika na adhabu ya mwenyezi Mungu au hali ya kuokoka. Dhamira hii imejitokeza katika nyimbo ya Chrisstina Shusho iitwayo "Thamani ya Wokovu Wangu." Mungu kwa ajili ya wokovu, faraja, neema, amani, utakatifu na huruma. Kutokana na hayo, imedhihirika kwamba mwimbaji anamrejelea Mungu kuwa aliye mwadilifu kwa sababu yeye akikupenda wala hatoitoa kasoro na ukimpokea leo atabadili historia yako. Kwa mfano, tazama ubeti ufuatao:

> Maisha ni hazina iliyo mikononi mwa Mungu
> Hakuna ajuaye salio la siku zake
> Ukiona ni mzima leo hujui kesho itakuaje
> Ndio maana nimeamua nikukumbushe habari za yesu
> Yeye akikupenda wala hatoitoi kasoro,
> Ukimpokea leo atabadili historia yako (ub. 2).

Katika wimbo huu unaelezea uzuri wa kuwa na Yesu na sifa za Yesu na umuhimu wa wokovu. Ukiwa na Yesu hakuna la kukushinda na wala yeye hatoitoi kasoro kama wanadamu. Msanii huyu aliangalia maisha ya wanadamu akayaona yapo katika hali ya kupita hapa dunia. Anasema kuwa ili uwe wa thamani mbele za Mungu na wanadamu ni kuukubali wokovu kwa kumpokea na kumkiri Yesu Kristo kuwa Bwana na mwokozi wa maisha yako.

#### 4. 2. 3. 2 Hali ya Maisha

Maisha ni muda wa uhai wa kiumbe au namna ya kuishi. Utafiti umebaini kuwa dhamira inayopatikana katika nyimbo za Injili za Christina Shusho kuwa zinahusu hali ya maisha ya kila siku. Dhamira zinazopatikana katika nyimbo zake hugusa maisha ya watu na hivyo kusababisha watu kuvutiwa na nyimbo zake. Hii inathibitisha katika wimbo wa "Unikumbuke," mtunzi anasema:

> Maisha yangu, kazi yangu kuketi kwangu, nakuondoka kwangu
> unikumbuke
> Mnyonge mimi dhaifu mimi (unikumbuke)
> Ona huyu asie na kazi (unikumbuke)
> Yatima na wajane wanalia (unikumbuke)

Kijana huyu ataka mwenzi (umkmbuke)
Na mwingine huyu ataka elimu (unikumbuke)
Umasikini sasa ndio wimbo (unikumbuke)
Nchi nzima vilio vimejaa (unikumbuke) (ub. 2).

Hapa mtunzi anaelezea kuwa katika matatizo anayokumbana nayo binadamu amkumbuke Mungu, ili kuweza kutatuliwa matatizo yake. Kwa sababu Mungu pekee ndiye mtatuzi wa yote. Hali hii ipo katika jamii zetu ambayo inasababisha watu kukata tamaa ya maisha.

#### 4.2.3.3 Imani

Imani ni mambo anayokubali mtu kuwa ni ya kweli na anayopaswa kuheshimu, hasa katika dini. Nyimbo za Injili za Christina Shusho zina dhamira zinazochoma mioyo ya watu na kuwapa hisia inayowafanya wajihisi kuwa shida zao zimeisha na kujihisi kuwa wako katika ulimwengu mwingine. Mwimbaji anaona kuwa suluhisho la matatizo ya wanadamu anayokumbukana nayo ni kumwomba Mungu. Katika wimbo wa “Ee Bwana Umenichunguza”, mtunzi anasema:

Ee Bwana umenichunguza na kunijua
Wewe wajua kuketi kwangu nakuondoka kwangu
Umenifahamu wazo langu, tokea mbali
Umepepeta kwenda kwangu na kulala kwangu
Umeelewa na njia zangu zoote
Umepepeta kwenda kwangu, nakulala kwangu
Umeelewa njia zangu zoote (ub. 1).

Mtunzi katika ubeti huu anasisitiza kuwa na imani na Mungu. Kutokana na kuwa Mungu ndiyo anayejua kila kitu unachofanya hapa duniani. Mtunzi anaendelea kueleza kuwa hata njia na mahali pa kulala kwako yeye ndiye anayejua.

#### 4.2.3.4 Wema na Huruma

Wema ni hali ya matendo mazuri na huruma ni moyo wa wema. Nyimbo za Christina Shusho zinaelezea umuhimu wa kutenda wema na kuwa na huruma kwa wengine. Pia, ili watu wawe karibu na Mungu waishi maisha ya kumcha na kumpendeza Mungu kila siku. Katika wimbo wa “Napenda,” mtunzi anasema:

Napenda neno lako
Napenda hekima zako
Napenda sifa zako yesu
Kila kitu kwako mimi napenda
Napenda hukumu zako
Napenda huruma zako
Napenda rehema zako
Kila kitokacho kwako mimi napenda (ub. 3).

Ubeti huu unafafanua kuhusu wema na huruma ya Mungu kwa binadamu. Mungu katika kutoa maamuzi juu ya binadamu hana upendeleo kwa mtu yeyeto. Hivyo, upendo, huruma, hukumu na hekima kwa binadamu wote ni sawa.

#### 4.2.3.5 Ndoa

Ndoa ni makubaliano rasmi ya mwanamke na mwanaume kuishi pamoja kama mume na mke. Dhamira ya ndoa inahusu mwanamke na mwanaume kuwa na wajibu wa kulinda ndoa yao, hasa kwa maombi ili ndoa yao iwe na amani na furaha wakati wote. Katika wimbo wa "Adamu," mtunzi anasema:

Mwanamke ataacha wazazi wake, ataandamana na mume
Mwanaume ataacha wazazi wake, ataandamana na mkewe
Hao wawili watakuwa mwili mmoja, wanie mamoja washirikiane kwa umoja x2 (ub. 2).

Ubeti huu unaelezea kuwa kuna umuhimu wa wanandoa kushirikiana katika kila jambo. Kitendo hiko kitasababisha ndoa hiyo kudumu na kuendelea kumuabudu Mungu. Hapa tunaona kuwa hata katika jamii zetu ndoa inahitaji ushirikiano wa kutosha kutoka kwa wanandoa wote wawili.

#### 4.2.3.6 Ukombozi

Ukombozi ni uokoaji wa watu kutoka kwenye hali mbaya ya udhalimu au hali duni. Dhamira hii imejitokeza katika nyimbo za Christina Shusho kutokana na ukweli kuwa binadamu tunaitaji ukombozi kutoka kwa Mungu. Hii inatokana na mambo mabaya

tunayoyafanya na kujikuta tukimkosea Mungu. Katika wimbo wa “Ee Bwana Utete Nao”, mtunzi anasema:

Uimbie nafsi yangu
Mimi ni wokovu wako
Waambishe, wafedheheshwe
Wanaoitafuta nafsi yangu
Warudishwe nyuma
Wafadhaishwe
Wanonizushia mabaya x2
Wawe kama makapi
Mbele ya upepo
Malaika wa Bwana
Akiwafuatia x2 (uk. 3).

Hapa mtunzi anasisitiza mtu kuomba ukombozi kutoka kwa Mungu, ili aepushe na mabaya kutoka kwa watu wanaomuombea mabaya.

#### 4.2.3.7 Nguvu na Utukufu wa Mungu

Dhana ya nguvu inarejelea uwezo wa kufanya jambo huku neno utukufu likirejelea ile hali ya kutukuka. Wimbo wa Christina Shusho unaelezea kuwa kuna umuhimu wa kumuabudu na kumuomba Mungu kwa kila jambo. Mungu ni mtakatifu na anastahili utukufu wote kwa maana hata malaika mbinguni humsujudu na kumwabudu. Katika wimbo wa “Wastahili Kuabudiwa”, mtunzi anasema:

Wakuabudiwa, wakuheshimiwa niwewe Mungu
Wakupewa sifa, nautukufu ni wewe Mungu
Mungu mwenye nguvu, wastahili heshima zote
Hakuna mwingine,wa kulinganishwa na wewe Mungu x2 (ub. 1).

Ubeti huu unaelezea kuwa binadamu tunapaswa kumuabudu na kumuheshimu Mungu. Kwani Mungu ndiye pekee anayepaswa kuabudiwa na kuheshimiwa, hivyo sifa zote zielekezwe kwake na si kwa mwingine yoyoyte.

Dhamira ya nyimbo za Injili zinafanana na tanzu nyingine za fasihi ingawa nyimbo za Injili zinatumia maandiko matakatifu kutoka katika Biblia ila utunzi wao unafuata mabandiliko ya jamii. Jamii ikibadilika kutokana na sayansi na teknolojia pia, na nyimbo

zao hubadilika kwa sababu waimbaji au wasanii ni kioo cha jamii. Hivyo, huendana na mabadiliko ambayo jamii inayapitia na hugusa maisha ya watu kwa kiasi kikubwa.

### 4.3 Upokezi wa Nyimbo Za Christina Shusho kwa Jamii ya Watanzania

Hapa kunaelezea upokezi wa nyimbo za Injili kwa ujumla na upokezi wa nyimbo za Injili za Christina Shusho.

#### 4. 3. 1 Upokezi wa Nyimbo za Injili kwa Ujumla

Utafiti umebaini kuwa, nyimbo za Injili zinapokelewa kwa kiasi kikubwa sana katika jamii ya Watanzania. Hii imetokana na uamsho wa watu miaka ya hivi karibuni kutambua nguvu ya Mungu iliyoko ndani ya nyimbo hizo. Na nguvu hizo mara nyingi huwa zimebeba dhamira zinazohusu maisha ya watu kwa jumla. Hali hii imesababisha kupendwa kwa nyimbo za Injili kwasababu ni nyimbo zinazoendana na maisha ya kila siku. Kuwepo kwa matamasha mengi ya nyimbo za Injili hivi sasa ndiyo kunasababisha watu kupokea nyimbo hizo kwa kiasi kikubwa. Picha ifuatayo inaonyesha watu wakiwa kwenye tamasha la Injili la Krismasi lililofanyika tarehe 25/ 12/2015 jijini Dar es Salaam.



Mashabiki wa nyimbo za Injili wakiwa katika tamasha la Krismasi jijini Dar es Salaam (Utafiti, 2016)

Nyimbo za Injili zinapokelewa kwa sababu ni muziki ambao unaeleweka na wasomi na wasio wasomi na nyimbo hizi hupokelewa na watu wa rika zote. Pia, kutokana na ujumbe uliomo na namna msanii alivyoweza kugusa jamii yake inayomzunguka. Kama tujuavyo kuwa fasihi ni zao la jamii, kwa hiyo, msanii hana budi kutunga kazi zinazogusa jamii katika nyanja zote ili ziweze kuwagusa wapokezi.

Vilevile, nyimbo za Injili hupokelewa kwa kiasi kikubwa na watanzania kwasababu, uimbaji ni sehemu mojawapo katika huduma yao kama washabiki mbalimbali wa michezo wa mpira wa miguu. Kwa hiyo, nyimbo za Injili husaidia kuchochea ibada, kufariji misiba na hata kusherehesha wakati wa sherehe mbalimbali kama vile: arusi, kipaimara, ubatizo na komunio. Hivi vyote ni vitu ambavyo hutokea katika jamii zetu kila siku. Kwa hiyo hapa tunaona jinsi nyimbo za Injili zinavyopokelewa vizuri miongoni mwa jamii ya Watanzania.

Pia, nyimbo za Injili zinapokelewa kwa kiasi kikubwa na hasa nyimbo za kuabudu kuliko za kuruka sana kwa mitindo mingi. Kwa sababu nyimbo za kuabudu zinavuta uwepo wa Mungu haraka kuliko nyimbo za kuruka ruka. Waliendelea kusema kuwa watu wanazipokea kwa wingi nyimbo za Injili kwasababu zinawagusa kiroho, hutoa ujumbe halisi kwa mifumo yote ya maisha. Kwa hiyo, katika utafiti huu, mtafiti aliweza kukubaliana na wanazuoni mbalimbali ambao wanasema kuwa nyimbo za Injili ni kipera kimojawapo cha fasihi simulizi kama asemavyo Mulokozi (2003).

Kwa upande mwingine mtafiti amebaini kuwa nyimbo za mwimbaji huyu wa Injili zinapokelewa kwa wastani miongoni mwa jamii ya Watanzania kwa sababu ya hali halisi. Watu wengi wanapenda nyimbo za bongo fleva sana kuliko za Injili. Pia, baadhi ya waimbaji wenyewe wanasababisha nyimbo za Injili zisipokelewe sana kutokana na jinsi wanavyoonekana hasa uvaaji na uchezaji kama wa muziki wa kidunia. Hii ni kutokana na

mabadiliko ya sayansi na teknolojia yaliyosababisha kuwepo kwa mitindo mipya ya uvaaji na uchezaji unaoendana na wakati ulimwengu unaopitia sasa na ndio chanzo kilichosababisa waimbaji wa nyimbo za Injili kucheza na kuvaa kama waimbaji wa nyimbo za kidunia.

Pia, nyimbo za Injili hapa nchini zinapokelewa kwa kiasi kidogo kulinganisha na nchi za nje. Hapa nchini tunaandaliwa tamasha moja la Injili kwa mwaka wakati wenzetu wa nchi za nje wanakuwa na matasha mengi na pia nyimbo za kidunia zinakuwa na matamasha mengi hapa nchini, ndiyo sababu inayowafanya watu wapende nyimbo za kidunia zaidi.

### 4.3.2 Upokezi Wa Nyimbo Za Injili Za Christina Shusho

Utafiti umebaini kuwa nyimbo za mwimbaji huyu zinapokelewa kwa kiasi kikubwa sana na wapenzi wa nyimbo za Injili nchini Tanzania kutokana na jinsi mwimbaji huyu anavyojua kuimudu na kuitumia sauti yake vizuri inayowavutia watu wengi. Kwa kushadidia hili mtengenezaji wa nyimbo za Injili wa studio ya Shusho iliyoko Segerea mwisho jijini Dar es salaam alisema:

> Christina Shusho ni mwimbaji ambaye anajua kuitumia sauti yake vizuri, anaimba kwa sauti yake halisi haweki madoido na hivyo kumfanya kuimudu sauti yake halisi ambayo inavutia sana.

Vilevile utafiti umebaini kuwa nyimbo za Injili za Christina Shusho zinapokelwa kwa wingi na wasikilizaji na wapenzi wa nyimbo za Injili nchini kwasababu ya ujumbe ambao umo katika nyimbo zake zinazogusa hali halisi ya maisha ya watu na hivyo kuwafanya wazipokee kwa wingi licha ya kujua kuimudu sauti yake vizuri. Kuthibitisha hili Musiba alisema:

> Shusho ni mwimbaji wa nyimbo za Injili anayejua kuitumia sauti yake vizuri ambayo inawavutia wasikilizaji wengi na anajua kupangilia ujumbe unaoendana na wakati yeye hubadilika kutokana na wakati ndio maana nyimbo zake zinapendwa.

Pia, shusho ni mwimbaji anayebadilika katika ujumbe wa nyimbo zake ambazo hugusa maisha ya watu na hubadilika kutokana na mazingira.

Vilevile shusho ni mwimbaji mwenye mahadhi ya tofauti na waimbaji wengine amabyo huwafanya watu wazipokee nyimbo zake kwa wingi. Nyimbo zake nyingi zina mahadhi ya kumbembeleza tofauti na wasanii wengine. Kwa kushadidia hili msichana wa jijin dar es salaam alisema:

> Christina Shusho ni mwimbaji mwenye mahadhi ya kumbembeleza tofauti na waimbaji wengine wa nyimbo za Injili. Nyimbo zake hubenbeleza na huvutia watu kuzisikiliza mara kwa mara na kusababisha watu kuzipokea kwa wingi.

Pia utafiti umebaini kuwa, watu wanapokea nyimbo za Injili za Christina Shusho kwa wingi sana kutokana na kwamba mwimbaji huyu anaimba nyimbo zake katika hali ya usafi. Hapa utafiti ulimaanisha usafi wa moyo na usafi yaani kuwa na tabia nzuri zinazompendeza Mungu na nikitu kimojawapo kinachopelekea watu wazipokee kwa wingi nyimbo za mwimbaji huyu. Kwa kushadidia hili mama mmoja alisema:

> Christina shusho ni mwimbaji anayeimba kwenye hali ya usafi na ana sauti nzuri sana ya tofauti amabayo ni kivutio kikubwa sana kwa wapenzi wa nyimbo za Injili.

Vilevile utafiti umebaini kuwa upokezi wa nyimbo za Christina Shusho kwa watanzania niwa hali ya juu sana hii ni kutona na jinsi mwimbaji huyu anavyoweza kucheza vizuri kistaraabu, melodi ya nyimbo zake, lugha anayoitumia niya kuvutia, mitindo ya uimbaji wake pamoja na vitu vinavyofanana na hivyo.

## 4.4 Sababu za Kupendwa kwa Nyimbo za Injili kama Fasihi Pendwa

Sababu za kupendwa kwa nyimbo za Injili kama fasihi pendwa ambao walijibu swali hili kama ifuatavyo, watayarishaji wa nyimbo walisema nyimbo za Injili zinapendwa sana kwasababu ya uwasilishaji wake, namna zinavyochezwa, ujumbe, zinaelimisha, zinafundisha, zinashawishi mtu kuacha mabaya na pia ni nyimbo ambazo hupendwa na

rika zote. Nyimbo za Injili zinapendwa kwasababu ya mtindo wa uchezaji wake, namna mwimbaji anavyoimba na kuweza kuitawala jukwaa ambao huwavutia watu waendelee kupenda zaidi. Namna wasanii wanavyocheza nyimbo hizo husababisha watu waendelee kuzipenda na kuvutiwa nazo zaidi.

Vilevile, ujumbe wa neno la Mungu unaopatikana katika nyimbo hizo. Kuna watu wengine wanapenda kusikiliza nyimbo za Injili na hupata kitu hata kama hawajaenda kanisani. Hata hivyo, suala hili linasababisha kuwepo kwa sababu ya kupendwa kwa nyimbo za Injili tofauti na zamani na kusababisha kipera hiki cha nyimbo za Injili kupata mashiko kwa kasi kubwa katika jamii. Kijana alisema:

> Ujumbe wa neno la Mungu kuna watu wengine wanapenda kusikiliza nyimbo za Injili na wanapata kitu hata kama hajaenda kanisani. Anaendelea kusema kusema kuwa hata mimi huwa siendi kanisani lakini Napata ujumbe wa neon la Mungu kupitia nyimbo za Injili ninazo sikiliza kila siku.

Pia, zina ustaraabu pamoja na kufundisha watu kuliko nyimbo za muziki wa dunia. Kutokana na kuwa nyimbo za injili hazitumii lugha chafu na huzungumzia habari za Mungu za kuwaleta watu kwa Mungu. Vilevile, kiongozi wa dini alitoa sababu ya kupendwa kwa nyimbo za Injili kuwa ni nyimbo zenye nidhamu na zinazowavuta watu kuja kwa Mungu na kuacha maovu. Hapa tunaona jinsi nyimbo za injili kama fasihi pendwa zinavyotumia lugha nzuri isiyo na matusi na ni nyimbo zinazosikilizwa na watu wa rika zote kwa sababu zinaustaraabu ndani yake Mchungaji alisema:

> Watu wanapenda nyimbo za Injili kwasababu ni nyimbo za ustaarabu, zinafundisha watu kuliko muziki wa dunia sababu nyimbo za injili hutumia lugha nzuri. Pia huzungumzia habari za Mungu za kuwaleta watu katika ufalme wa Mungu.

Sababu nyingine za kupendwa kwa nyimbo za Injili ni kutokana zinahubiri habari njema za Yesu ili watu wapate kumjua Mungu, pia zinawajenga roho zao ili waweze kumjua Mungu, na kumpa Mungu utukufu. Aidha, sababu nyingine za kupendwa kwa nyimbo za

Injili kama fasihi, ni kama zifuatazo: Kwanza, ni kuwa muziki wa Injili unabeba kusudi la Mungu ndani yake la kuwafanya watu waokolewe. Pili ni ajira inayompatia maslahi msanii na tatu ni aina ya muziki ambao haubagui dini, dhehebu wala jinsia ukilinganisha na muziki mwingine. Kiongozi alisema:

> Kwanza muziki wa injili unabeba kusudi la Mungu ndani yake la kuwafanya watu waokolewe, Kwa ambaye anaufanya kwa maslahi ya Mungu mwenyewe. Pili, muziki huu ni muziki ambao haubagui dini, rika na dhehebu wala jinsia.

Vilevile, watu wanapenda nyimbo za injili kwasababu ni nyimbo zenye kutoa faraja, zinamguso mkubwa na ni nyimbo zenye matumaini kwa jamii ambazo zilikosa matumaini. Nyimbo za injili nyingi zinagusa maisha ya watu na zinatoa faraja kwa jamii iliyokata tamaa. Musiba alisema;

> Watu wanamtafuta Mungu kwa njia nyingi na nyimbo ni njia mojawapo inayobeba ujumbe unaopenya haraka kuliko kitu kingine kwa haraka. Kama nilivyosema, binadamu wa sasa wanahitaji matumaini na faraja maana watu wanahitaji kufarijiwa na kupata matumaini. Kumbuka dunia tunayoishi ni dunia iliyokosa matumaini, kwahiyo ujumbe unaobebwa katika nyimbo za Injili unagusa roho za walaji kwa haraka zaidi, kwa hiyo ni hitaji la walaji.

Kwa mantiki hii, watu wanapenda nyimbo za injili kwa sababu ni nyimbo zinazogusa maisha yao na zinawapa faraja na matumaini wale waliokata tamaa na ndio maana watu mbalimbali wanazipenda na kusababisha waimbaji wa nyimbo za injili waongezeke kila siku. Hata tukija kwa upande wa fasihi pendwa, ni fasihi iliyotofauti na fasihi nyingine kwasababu hulenga kuwaburudisha watu nasio kuwavunja moyo.

Utafiti ulibaini zaidi kuwa sababu za kupendwa kwa nyimbo za Injili kama fasihi pendwa ni kutokana na kuwa na hofu ya Mungu. Yaani, ni kwa sababu nyimbo hizo huhubiri habari njema za Yesu ili watu wapate kumjua Mungu. Vilevile, zinajenga roho za watu ili na wao waweze kumjua Mungu. Pia wanapenda nyimbo za Injili kwasababu ya namna mwimbaji anavyoziwasilisha akiwa jukwaani, uvaaji wake na namna mwimbaji

anavyoitumia sauti yake vizuri katika kufikisha ujumbe kwa jamii. Kwa kuthibitisha hili kijana alisema:

> Watu wengi hivi sasa wamekuwa na hofu ya Mungu ndio maana watu wanapenda nyimbo za Injili. Hii ni kutokana kwamba, maovu yamezidi dunia kwahiyo watu wamekuwa na hofu ya Mungu ili kujiepusha na maovu yaliyopo.

Pia, sababu nyingine ya watu kupenda nyimbo za injili kuwa ni nyimbo zilizobeba neno la Mungu, wasikilizaji hupokea ujumbe wa moja kwa moja bila kuchoka, ni kiburudisho na ni sanaa yenye nidhamu ambayo husababisha watu wa rika zote na umri tofauti kupenda nyimbo. Vilevile, kiongozi mwingine wa dini alisema watu wanapenda nyimbo za dini kwasababu ya ujumbe na mafundisho yaliyomo katika nyimbo hizo za dini. Pia kiongozi mwingine wa dini alimweleza mtafiti kuwa, watu wanapenda nyimbo za dini kwasababu zinagusa roho za watu, hutoa ujumbe halisi kwa mifumo yote ya maisha. Hapa mtafitiwa alionyeshakwa namna gani nyimbo za dini huelezea au huzungumzia hali halisi za maisha ya watu katika jamii kama ilivyosifa mojawapo ya fasihi pendwa kuwa ni kuzungumzia na kugusa hali halisi za maisha ya watu katika jamii na kitu cha pekee kinachowafanya watu wazidi kupenda. Akishadidia jambo hili mchungaji wa Anglican Dodoma anasema:

> Watu wanapenda nyimbo za injili kwasababu niza neno la Mungu, wasikilizaji hupokea ujumbe wa moja kwa moja bila kuchoka, ni kiburudisho na ni sanaa yenye nidhamu.

Kama tulivyoona katika nadharia ya upokezi ambayo inaeleza kuwa maana ya kazi iko kwa msikilizaji au hadhira ndivyo ilivyo kwa nyimbo za Injili. Msingi mkubwa wa nadharia hii kuwa uhai wa kazi wa fasihi unategemea uhusiano na maingiliano baina ya matini yenyewe na yule anayeipokea. Kwa mantiki hii, watafitiwa wametoa sababu za kupendwa kwa nyimbo za Injili, kama fasihi pendwa kulingana na uhusiano wake na maingiliano bayana ya kazi ya sanaa ya uimbaji aliyoisikiliza na kuitazama na jinsi

alivyoipokea kazi hiyo na kupata ujumbe unaomfaa. Ndio maana kila mtafitiwa alitoa sababu zake kulingana na jinsi alivyoipokea na kuielewa kazi hiyo ilivyomgusa. Kwa hiyo, msingi huu wa nadharia hii ya upokezi ulimuongoza mtafiti kuweza kuchambua sababu za kupendwa kwa nyimbo za injili kutoka kwa watafitiwa.

**4. 5 Muhtasari wa Sura ya Nne**

Sura hii imewasilisha matokeo ya uchambuzi wa data zilizokusanywa kwa kuzingatia malengo mahsusi yote matatu ambayo yametokana na lengo kuu ya utafiti huu. Utafiti umeelezea mwelekeo wa maudhui wa nyimbo za Injili, Upokezi wa nyimbo za Injili kwa ujumla na upokezi wa nyimbo za Christina Shusho pamoja na kupendwa kwa nyimbo za Injili.

# SURA YA TANO

# MHUTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii ni inahusu kazi nzima ya utafiti uliofanyika juu ya misingi ya kupendwa kwa nyimbo za Injili kama fasihi pendwa kwa kuangalia nyimbo mbalimbali za mwimbaji wa nyimbo za Injili, Christina Shusho. Sura hii ina sehemu tatu ambazo ni mhutasari, hitimisho na mapendekezo.

## 5.2 Muhtasari wa Tasnifu

Utafiti huu ulilenga kuchunguza misingi ya kupendwa kwa nyimbo za injili kama fasihi pendwa kwa kuangalia nyimbo za Christina Shusho. Tumechunguza na kubainisha maudhui ya nyimbo za Injili za Christina Shusho zinavyolandana na jamii husika. Pia, tumechunguza sababu za kupendwa kwa nyimbo za Injili kutokana na kupata maoni mbalimbali kutoka kwa wadau wa nyimbo za Injili. Aidha, utafiti huu umeongozwa na nadharia ya upokezi.

Tasnifu hii ina sura tano: Katika Sura ya Kwanza, kuna usuli wa tatizo, tamko la tatizo, malengo, maswali, umuhimu na nadharia. Mapitio pamoja na mapengo yamejenga sura ya pili. Sura ya tatu imejengwa na mbinu za utafiti za ukusanyaji dada, uchakataji data, sampuli na mahali ulipofanyika utafiti. Mbinu ya kukusanya data maktabani na uwandani. Uwasilishaji na mjadala wa data katika kujenga sura ya nne ya tasnifu hii. Katika sura hii uchambuzi wamjadala wa misingi ya kupendwa kwa nyimbo za Injili umefanyika. Tasnifu imebaini kuwa nyimbo za Injili hususani za Christina Shusho zina ujumbe unaogusa wasikilizaji wa aina mbalimbali kwa namna ya kipekee. Pia, zinatoa masuhisho ya matatizo ya binadamu anayokumbana nayo na kuhamasisha watu wawe karibu na Mungu.

### 5. 3 Hitimisho

Hapa kunalenga kuelezea mambo mawili ambayo ni matokeo ya utoshelevu wa mkabala uliotumika pamoja na mchango mpya wa utafiti.

### 5. 3. 1 Utoshelevu wa Mkabala Uliotumika katika Utafiti

Mkabala uliotumika katika uchambuzi wa data za tasnifu hii ni upokezi. Msingi wa upokezi ni kuelezea fasihi kuwa maana na uhai wa kazi inategemea maingiliano baina ya mpokezi na kazi yenyewe. Kwa hiyo, mkabala wa upokezi umetuongoza katika kuchunguza hali ya kupendwa kwa nyimbo za Injili kama fasihi pendwa mfano kutoka katika nyimbo za Christina Shusho.

Pia, mkabala huu umetusaidia kuchunguza mwelekeo wa kimaudhui wa nyimbo za Injili za Christina Shusho. Hii imesaidia kubainisha nyimbo zake pamoja na mwelekeo wa kidhamira katika nyimbo za Christina Shusho. Kwa hiyo, nadharia ya upokezi imesaidia kubainisha dhamira zilizomo katika nyimbo za Christina Shusho.

Aidha, nadharia hii imesaidia kubainisha sababu za kupendwa kwa nyimbo za Injili katika jamii ya watanzania. Hivyo, imetuongoza katika kuelezea upokezi wa nyimbo za Injili kwa ujumla na katika nyimbo za Christina Shusho. Kwa hiyo, ni imani ya tasnifu hii kuwa matokeo ya utafiti huu una ubora ambao ulilengwa.

### 5. 3. 2 Mchango  Mpya wa Utafiti

Utafiti huu umengudua kuwa nyimbo za Injili ni kipengere kimoja wapo cha fasihi pendwa ndani ya fasihi simulizi, vilevile utafiti huu umengudua kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya wasanii, wasambazaji, watayarishaji na viongozi mbalimbali wa dini na serikali. Pia, utafiti huu umengudua kuwa watu wanapenda nyimbo za Injili kutokana na naman msanii wa nyimbo za Injili anavyoonekana na anavyoimba**.**

### 5.4 Mapendekezo

Utafiti huu ulilenga hali ya kupendwa kwa nyimbo za Injili kama fasihi pendwa. Hivyo, inapendekeza kuwa waatalamu wa fasihi simulizi wachunguze zaidi utanzu wa nyimbo, hususani nyimbo za Injili katika kipengele cha fani na maudhui. Pia, inapendekeza kuwa ufanyike utafiti wa kina kuhusu waimbaji wa nyimbo za Injili wakati wa kusana kazi zao. Aidha, wachunguzwe watayarishaji wa nyimbo za Injili inawezekana kuwa hawana ujuzi wa kutosha wakati wa kutengeneza nyimbo hizo. Vilevile, viongozi wa kijamii na kisiasa waweza kutoa ushirikiano wa kutosha katika kuendeleza nyimbo za Injili.

.

## MAREJELEO


Adedeji, F (2004), “Classification of Nigerian Gospel Music Styles” katika *Nigeria Music Review*, Juzuu ya 5.

Anderson, W. (1977), *The Church In East Africa*, Dodoma-Tanzania Central Tanganyika Press, Dodoma.

Baradyana, J. S na Ame, A (2007), “IM 205: *Business Research Methods*” (Course material), University of Dar es salaam.

Barz, G. (1997), “The Performance Of Religion And Social Identity An Ethnography Of Post- Mission Kwaya Music In Tanzania East Africa,” Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Brown, (Haijachapishwa).

Barz, G. (2003), “Perfoming Religion, Negotiating Past and Present in Kwaya” katika *Music of Tanzania Review*, Juzuu ya 42.

Bitende, I. F. (2012), “Taswira za kidini katika riwaya za E. Kezilahabi,” Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).

Dickson A. W. (2006), *The Brief Of History Of Christian Music*. Oxford Press, England.

Finnegan R. (1997), *Oral literature in Africa*, Oxford University Press, London.

Johnson, B (2008). *A Change Is Gonna Come: The Transformation Of Traditional To A Contemporary Worship Celebration*, Authorhouse, New York

Khamis, S. A. (2007), “Vionjo vya Riwaya Mpya ya Kiswahili katika,” katika *kioo cha Lugha*, Juzuu ya 5. TUKI, Dar es Salaam.

Kidula.J. (2000), “Polishing the Luster of the Stars, Music Professionalism Made Workable Mkenya.” katika *Ethno Music Cology*, Juzuu ya 44 (3) uk. 408-428.

Kitundu, A (2011), “Athari za Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia Kwenye Fasihi Simulizi: Nyimbo za Ibada ya Dini ya Kikristo Tanzania,” Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu ya Sanaa katika Fasihi, Chuo Kikuu Cha Dodoma, (Haijachapishwa).

Kothari, C. R. (2009), *Research Methodology: Methods and Technigues,* (2nd ed), (New Age International Publishers Ltd, New Delhi.

Kweka, E.S. (2013), “Uchambuzi wa Dhamira Katika Nyimbo za Muziki wa Injili Dar es Salaam,” Tasnifu ya Shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, (Haijachapishwa).

Mkallyah, A. K. (2011), "Affected And Effects of Musical Attributes and Cultural Usage of Indigenous Tanzania Music Traditions in Church Worship" Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa).

Mulokozi, M. M (1996), *Moto wa Mianzi*, Ecob publications, Morogoro

Mushengezi, A. (2003), *Twenty Century Literary Theory*, Makerere University, Kampala.

Mwavika, M (2011), "Nafasi za Fasihi Katika Ibada za Dini za Kikristo." Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu ya Sanaa katika Fasihi, Chuo Kikuu Cha Dodoma (Haijachapishwa).

Perullo, A. (2011), *Live from Dare S Salaam Popular Music and Tanzania Music Economy*. Indian University Press, New York.

Ponera, A. S. (2014), *Utangulizi wa Nadharia: Fasihi Linganishi*, Karljamer Print Technology, Dar es Salaam.

Raymond, (2002), "Blacks Gaspel Music" Tasnifu ya Shahada ya Uzamili Chuo Kikuu cha Colombia (Haijachapishwa).

Sanga, I. (2006), "Muziki wa Injili: The Temporal and Spatial Aesthletics of Popular in Dar es salaam, Tanzania (1980-2005)" Tasnifu ya Shahada ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kwazulu –Natal (Haijachapishwa).

Sanga, I. (2007), "Gender In Church Music: Dynamic of Gendered Space in Muzik wa Injili in Dar es salaam". katika *Journal of Popular Music Studies*, Juzuu ya 19 (1) uk. 59.

Shulman, R. (1988), *Contemporary Methods for Research Education: American Education Research Association* TUKI, Dar es salaam.

TUKI (2004), *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Dar es Salaam.

Wafura, R. M na Njogu, K (2007), *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*, Sai Industries Limited, Nairobi.

Wamitila, K .W (2002), *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*, Phoenix Publishers Limited, Nairobi.

Wamitila, K. W. (2003), *Kichocheo Cha Fasihi: Andishi na Simulizi*, Focus Books, Nairobi.

Williams, J. (1972), *East Africa History*. Longman Kenya Ltd, Nairobi.

# VIAMBATANISHO

## A Miongozo ya Usaili

### A. 1 Mwongozo wa Usaili kwa Christina Shusho

Utafiti huu unahusu misingi ya kupendwa kwa nyimbo za injili kama fasihi pendwa. Lengo la utafiti huu ni kuibua misingi ya kupendwa kwa nyimbo za injili kama fasihi pendwa. Kujua sababu za kuwepo kwake, pamoja na kujua kwanini mwimbaji huyu nyimbo zake zinapendwa. Pia utafiti huu unalenga katika kujua misingi ya kupendwa kwa nyimbo pendwa za injilkama fasihi pendwa.

1. Katika utafiti huu, nyimbo za Injili zinachukuliwa kuwa ni zile nyimbo ambazo zinawavutia watu wengi na wanapenda kuzisikiliza. Una maoni gani kuhusu mtazamo huu au maana hii?
2. Watu hupokeaje nyimbo zako?
3. Sababu zipi inayopelekea kupendwa kwa nyimbo za injili?
4. Mpaka sasa una alubamu gapi za nyimbo za injili?
5. Kuna aina gapi za nyimbo za injili? Wewe unaimba aina gani?
6. Una maoni gani kuhusu ukuaji wa nyimbo za injili kama fasihi pendwa?
7. Unaweza kuelezeaje kuhusu kuwepo kwa sababu au kutokuwepo kwa sababu ya kupendwa kwa nyimbo za Injili kama fasihi pendwa?
8. Nini dhamira ya nyimbo zako?

**A. 2 Mwongozo wa Usaili kwa wadau wa Nyimbo za injili**

1. Tunaomba utueleze kwa ufupi kuhusu jina na umri wako.

2. Je! Unamjua Christina Shusho? Kama ndio eleza umjuavyo.

3. Nyimbo za Injili unazipokeaje?

4. Katika nyimbo zake hizo, unaweza kukumbuka ni kitu gani kilikusukuma mpaka ukaupenda?

6. Kuna aina gapi za nyimbo za injili?

7. Una maoni gani kuhusu sababu ya kupendwa kwa nyimbo za Injili za kama fasihi pendwa?

8. Nyimbo za Injili zina dhamira gani?

**B. MATUKIO YANAYOHUSIANA NA NYIMBO ZA INJILI**




Picha 1: Wapenzi wa Nyimbo za Injili wakiwa kwenye Tamasha la Christina Shusho (Utafiti, 2016)




Picha 2: Mwimbaji Christina Shusho akiwa jukwaani picha kutoka mtandaoni



Picha 4: Wapenzi wa nyimbo za Injili wakiwa kwenye tamasha la Twenzetu kwa Yesu (picha mtandaono)



Picha 5: Mtafiti (kulia) akiwa na Mtayarishaji wa nyimbo za Injili (Utafiti, 2016)